
**Mabasi** yazuiwa kubeba abiria sababu ya ubovu UKURASA 2



**Akutwa** amejinyonga kwa chandarua madai kukimbiwa mke, watoto UK. 7



**Maaskofu** DRC waweka msimamo ndoa za jinsia moja UK. 19



**GERRARD NJIA PANDA AL-ETTIFAQ**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Desemba 27, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581537

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




# Kimaro akemea viongozi maslahi

• **Awataka** kuacha kuwaza uchaguzi, wajenge taifa la kesho *Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### MIKOA 15 YAHADHARISHWA KUNYESHA MVUA YA MAFURIKO




MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA) imetoa tahadhari ya uwapo wa mvua kubwa inayotarajia kunyesha katika mikoa 15 inayoweza...

**RIPOTI MAALUM**

## Jongowe: Kijiji kisiwani kisicho na huduma uzazi

UKURASA 4



Mwanasheria wa Kikosi cha Usalama Barabarabi nchini, Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP), Deus Sokoni akiangalia namba za usajili za mabasi yaliyozuiliwa kuendelea na safari jana katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha mkoa wa Mbeya baada ya kubainika kuwa ni mabovu, kulia ni Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa wa Mbeya, Mrakibu wa Polisi Hussein Gawile. **PICHA : NEBART MSOKWA**

## Wadau siasa washauri watoto wanolewe uongozi kuleta usawa

UK. 3



Qailah Bilal



Simba Silaa



Isack Nchemba

**MICHEZO** **SERIKALI YATAKIWA 'KUIBEBA' RIADHA** UK.20

**MAONI, KATUNI** UK.6



Katibu Tawala Mkoa wa Singida,Dk. Fatuma Mganga, akimkabidhi mjasiriamali Emmy Gervas seti ya vifaa vya saluni, ambavyo vilitolewa na Shirika lisilo la kiserikali la Brac Maendeleo Tanzania (BMT) vilivyotolewa kwa wajasiriamali 902 wa wilaya za Manyoni na Singida DC juzi. Vitu vingine vilivyotolewa na shirika hilo ni cherehani, kuku ,ng'ombe na vifaa vya umwagiliaji, kushoto ni Ofisa Maendeleo ya Jamii Manispaa ya Singida, Hana Churi, aliyesimama nyuma ni Meneja wa Mkoa wa BMT, Isihaka Mirambo. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# Kimaro aonya viongozi wanaowaza uchaguzi badala ya kujali jamii

**Na Romana Mallya**

MCHUNGAJI Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT), Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, ameonya viongozi, vijana na 'machawa' kuacha kuendekeza kuridhisha nafsi zao badala ya kuangalia maslahi ya kizazi kijacho.

Amesema kuna haja viongozi kuandaa msingi bora kwa ajili ya maisha ya kizazi kijacho badala ya kujikita kwenye maslahi binafsi.

Mchungaji Kimaro alisema hayo juzi wakati akihubiri katika Ibada ya Krismasi iliyofanyika Usharika wa Kijitonyama, huku akiwataka viongozi wasifikiri juu ya uchaguzi ujao bali mustakabali wa jamii hususan kizazi kijacho.

Alisema kama baadhi ya waasisi wa nchi mbalimbali barani Afrika, wakiwamo Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume, wangefikiri juu ya uchaguzi ujao na maslahi binafsi, nchi zisingekuwa zilipo sasa.

Dk. Kimaro aliwapa somo wanasiasa kuwa kama wanataka kudumu kwenye ulimwengu wa siasa, waachane na mawazo ya Herode ya kuua vizazi badala yake wafiriki kuzalisha kizazi kijacho chenye tija kwa jamii na taifa kwa ujumla.

"Fikiri juu ya vizazi vijavyo. Ukija kanisani utakuta wachungaji na maaskofu mpaka wanakufa wanafikiria kizazi kijavyo. Ukija kwenye nchi, Mzee Karume na Mzee Nyerere (akimaanisha waasisi wa taifa) waliwaza juu ya kizazi vijavyo. Farao alikufa kwenye Bahari ya Shamu, Herode alikufa ovyo tu kwa sababu waliwaza uchaguzi na maslahi binafsi," alikumbusha.

Katika mahubiri yake, Mchungaji Kimaro alimsimamisha Mbunge wa Makete, Festo Sanga, aliyekuwapo ibadani hapo ambaye ni miongoni mwa waumini kanisani hapo, akitoa mfano akisema yeye na wengine watakaoelewa ndani ya nchi ya kwamba si uchaguzi ujao bali kizazi kijacho, watabarikiwa.

"Viongozi wa kanisa, viongozi wa taasisi mbalimbali ambao watasimama kuangalia kizazi kijacho wamebarikiwa na walio hai na waliokufa na watakaozaliwa wataendelea kuwabariki," alisema.

"Vijana acheni kuangalia uchaguzi. Ukiwa kiongozi alafu unawaza juu ya kitu yaani nafasi ijayo, yaani mimi Mchungaji Kimaro ninaacha kuwaza juu ya kujenga Kijitonyama, namna ya kuwafikia wenye mateso, maendeleo ya usharika huu, ninawaza mimi nitakuwa Mkuu wa Jimbo, mimi nitakuwa Askofu, huoni huo ni uwendawazimu?" alihoji huku akisema mtu akiwaza juu ya kizazi kijacho hawezi kuwa chawa. "Kuna chawa wa uchaguzi ujao na nafasi ijayo. Akimendea nafasi utakuta anaweka sumu, anatengeneza vitu vya sumu. Lakini anayewaza kizazi kijacho, akiamka asubuhi, ni kizazi kijacho mwanzo mwisho," alisisitiza.

Mchungaji Kimaro aliwaombea waumini wa madhehebu yote, wahakikishe wasiue kizazi kijacho kwa sababu ya kiti kama alivyofanya Herode.

"Kuna watu huko kazini wamepigika. Kuna watu wanafanyiwa fitina, kuna fujo za ajabu zinafanyika kwenye taasisi kwa nini? Wanahangaika na nafasi ijayo, na mimi nionekane. Ukitaka kuonekana rudi kwa Mzee Karume, rudi kwa Mzee Nyerere uone falsafa yao utaonekana tu. Ukitaka kuonekana rudi kwa viongozi waliotangulia utaonekana tu, waliangalia kizazi kijacho.

"Yeyote anayeangalia kizazi kijacho uwe na hakika ardhi ya nyumbani kwenu kulikozikwa kitovu chako itakuja tu, kwa nini? Hata baba zako waliolala wataungana kukuunga mkono kwenye kizazi kijacho, madhabahu itakuunga mkono, kwa nini?

"Kwa maana wenye heshima, wapakwa mafuta wa Mungu waliosimama kwenye madhabahu za Afrika waliangalia kizazi kijacho. Huna haja ya kwenda kwa mganga wa kienyeji, huna haja ya kuwa chawa, ukiangalia kizazi kijacho ardhi ya Afrika itakutetea.

"Ole wako uwe kiongozi ambaye unaangalia uchaguzi ujaona hutaki kizazi kijacho. Usipoangalia kizazi kijacho ukangalia nafasi ijayo, uteuzi ujao, viongozi wa Afrika waliolala na walio hai, na ardhi ya Afrika iliyopokea machozi ya ukombozi wa Afrika, iliyopokea damu ya ukombozi wa Afrika itakupiga," alionya.

# Mikoa 15 yatahadharishwa kunyesha mvua ya mafuriko

**Na Jenifer Gilla**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa (TMA) imetoa tahadhari ya uwapo wa mvua kubwa inayotarajia kunyesha katika mikoa 15 inayoweza kuleta athari ya mafuriko.

Mikoa iliyotajwa ni Kagera, Geita, Mwanza, Shinyanga, Tabora, Kigoma, Katavi, Dodoma, Singida, Rukwa, Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa na Kusini mwa Mkoa wa Morogoro.

Taarifa iliyotolewa na TMA juzi, ilisema mvua hiyo inaweza kuleta kiwango cha wastani cha athari ikiwamo mafuriko, baadhi ya maeneo kuzungukwa na maji na kuharibu shughuli za kiuchumi.

Aidha, taarifa ilisema mvua ilitarajiwa kunyesha kwa siku tatu kuanzia jana hadi kesho katika mikoa hiyo na kuwambukusha wananchi kuchukua tahadhari na kujiandaa kwa kununua mahitaji ya muhimu na kuweka ndani.

Julai 29, mwaka huu, TMA ilitangaza ujio wa El-Nino katika kipindi cha msimu wa vuli iliyotatarajiwa kunyesha kuanza Oktoba hadi Desemba, mwaka huu na kutoa angalizo kuwa, inaweza kusababisha athari katika maeneo mbalimbali.

# Mabasi yazuiwa kusafirisha abiria kisa ubovu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MABASI matano yanayosafirisha abiria kati ya mkoa wa Mbeya na mikoa mingine, yamezuiwa kuendelea na safari baada ya kukaguliwa na kubainika mabovu na yanahatarisha maisha ya abiria.

Mabasi hayo yalizuiwa jana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, baada ya maofisa wa kikosi hicho kutoka makao makuu na wa Mkoa wa Mbeya kwa kushirikiana na maofisa wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kufanya ukaguzi wa kushtukiza alfajiri kabla hayajaanza safari.

Mbali na maofisa wa vikosi hivyo, pia wadau wengine wa usafirishaji walishiriki wakiwamo wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na mabalozi wa usalama barabarani

Mwanasheria wa Kikosi cha Usalama Barabarabi nchini, Mrakibu Mwandamizi (SSP), Deus Sokoni, ambaye aliongoza ukaguzi wa mabasi hayo, alisema lengo la ukaguzi huo ni kudhibiti ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikisababishwa na ubovu wa mabasi hayo.

SSP Sokoni aliyataja mabasi hayo kuwa ni basi la kampuni ya Msigwa lenye namba za usajili T. 441 DHZ ambalo linafanya safari kati ya Mbeya na Songea mkoani Ruvuma na Isamilo lenye namba za usajili T. 864 DSB linalofanya safari kati ya Mbeya na Mwanza.

Aliyataja mabasi mengine kuwa ni Turu Best linalofanya safari kati ya Mbeya na Singida, Ahmed lenye namba za usajili T. 252 AZU linalofanya safari kati ya Mbeya na Tanga na basi la Arusha Express lenye namba za usajili T.641 AGA.

"Pamoja na matatizo mengine, haya mabasi yote matano yana tatizo la mifumo ya breki ambao ni hatari sana.

Hatuwezi kuruhusu mabasi haya yaendelee na safari wakati mifumo hiyo ni mibovu, barabara zetu zina milima na miteremko mikali ambayo ni hatari," alisema Sokoni.

Alisema mabasi hayo yameondolewa namba za usajili mpaka yatakapokuwa yametengenezwa na kukaguliwa ndipo yataruhusiwa kuendelea na safari.

Sokoni alisema kwa mabasi ambayo matengenezo ni ya muda mrefu waliagiza madereva na mawakala kuwatafutia magari mengine na kwa yale mabasi ambayo matengenezo yalikuwa ya muda mfupi abiria walitakiwa kusubiri kwa mashar-ti ya kuhudumiwa na wamiliki wa mabasi.

Alisema wamiliki wa mabasi ambao mabasi yao yataendelea kuwa mabovu watachukuliwa hatua kali za kisheria kwa maelezo kuwa wanahatarisha maisha ya watu kwa makusudi.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani wa Mkoa wa Mbeya, Mrakibu wa Polisi Hussein Gawile, alisema wamekuwa wakiwasisitiza madereva kuyakagua kwanza mabasi yao kabla ya kuanza safari ili kama yatakuwa na mapungufu wayarekebishe mapema.

Alisema ukaguzi uliofanyika utakuwa endelevu na hatua kali zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya wamiliki wa magari ambao watakuwa wanashindwa kuyafanyia matengenezo magari yao.

"Tunawataka matajiri wanaoleta mabasi yao Mbeya wahakikishe magari yao yanakuwa imara na wanayafanyia matengenezo ya mara kwa mara, hizi hatua tunazozifanya ni kuwakumbusha wamiliki wajibu wao," alisema

Ofisa Leseni na Ufuatiliaji wa LATRA Mkoa wa Mbeya, Aman Masue, alisema wamiliki wa mabasi yote yaliyozuiwa kuendelea na safari, waliandikiwa faini na kuwataka wazilipe kwa mujibu wa sheria za mamlaka hiyo.

HABARI KITAIFA

# Wadau wa siasa washauri watoto wanolewe uongozi kuleta usawa

**Na Jenifer Gilla**

WADAU wa siasa wamewashauri wazazi na walezi kuacha kulalamikia nafasi za uongozi kwenye siasa kuchukuliwa na watoto wa viongozi badala yake wajikite kuwajengea uwezo na ujasiri watoto wao tangu wakiwa wadogo.

Wamesema ni lazima wawajengee watoto wao misingi ya kugombea nafasi za vyama wakiwa na umri mdogo ili zisichukuliwe na watoto wa viongozi au watu wenye umaarufu.

Ushauri huo umetolewa baada ya Umoja wa Vijana wa Chama cha Mapinduzi (UVCCM) kufanya uchaguzi wa viongozi chipukizi na baadhi ya nafasi za juu kuchukuliwa na watoto wa viongozi na watu maarufu na kuibua mjadala.

Mwanadiplomasia na Mchambuzi wa Siasa, Hamduni Maliseli, alisema wazazi na walezi wanawajibu wa kuwanoa watoto wao katika uongozi ili kuwajengea uwezo wa kugombea nafasi za chama na kuongeza ushindani.

Alisema watoto huwa wanavutiwa na shughuli wanazofanya wazazi wao na kama wakipewa nafasi, wanakuwa watendaji bora kuliko hata watangulizi wao, kwa sababu ya kushiriki kwa muda mrefu zaidi tena kwa vitendo.

Alisema watoto wa viongozi serikalini walioshinda katika kinyang'anyiro hicho si kwa sababu ya kupendelewa bali hawakupata wenzao wenye uthubutu zaidi yao na kuwa, waliopiga kura ni wanachama wa kawaida wa UVCCM.

Alisema watoto hao wamepikwa na wazazi wao kukijua na kukitetea chama na kujengewa ujasiri wa hali ya juu wa kugombea nafasi hizo ili waweze kuyatekeleza kwa vitendo yale waliofundishwa.

"Hivyo niwasihi wazazi na walezi waliopo ndani na nje ya vyama vya siasa, washirikisheni watoto wenu katika shughuli za uongozi na siasa, haijalishi wewe ni kiongozi au la, mjengee mtoto wako misingi ya kiuongozi katika chama, naye atasimama na mtoto wa kiongozi na kufanya vizuri," alisema Hamduni.

Alisema wanaolalamika kuwa watoto hao wamependelewa kutokana na nafasi za wazazi wao serikalini na katika chama wanakosea, kwa sababu mtindo wa uchaguzi umefanyika kwa kupiga kura kwa mujibu wa kanuni za chama.

"Ni kosa kubwa sana na fikra za ubaguzi kudhani kwamba watoto wa viongozi hawafai kuongoza katika chama.

"Kiongozi hazaliwi kuwa hivyo, bali anaandaliwa katika ngazi ya familia na kuja kuchaguliwa kwa mujibu wa kanuni za chama," alifafanua.

Akizungumzia malalamiko kuwa watoto hao hawakustahili kugombea nafasi hizo kwa kuwa wana umri mdogo, Maliseli alisema haoni tatizo lolote kwa sababu, maana halisi ya chipukizi ni vijana wadogo ambao wanalelewa kuja kuwa viongozi wakubwa baadaye.

"Maana ya chipukizi ni kuwa ni watoto wadogo, wanaoandaliwa kwa makusudi kwa mujibu wa chama ili baadaye waje kuwa watetezi, walinzi na viongozi wa baadaye wa chama," alisema.

Mchambuzi wa Siasa, Luaga Kizoka, alishauri somo la siasa kwa watoto litiliwe mkazo hata katika mazingira ya shule ili kuibua vipaji vya watoto kwenye uongozi na kuongeza idadi ya watoto wasio wa viongozi kugombea nafasi za chipukizi.

Alisema katika safari ya mtoto kisiasa suala la umri pia, lizingatiwe ili watoto hao waanze kupatiwa elimu ya uongozi shuleni kwa kugombea nafasi kama vile kiranja, dada na kaka mkuu, skauti na kiongozi wa timu.

Akifafanua kuhusu malalamiko kuwa walioshinda wengi ni watoto wa viongozi, Kizoka alisema sio jambo la kushangaza kwa sababu, watoto hao wamejifunza kupitia wazazi wao.

"Mara nyingi katika familia, mhamashishaji wa kwanza wa watoto wetu ni sisi wazazi, sisi ndio nyota inayowaongoza kwa hiyo, kuona watoto wa viongozi sio jambo la ajabu," alisema.

Aidha, alikishauri chama kulenga kuweka usawa wa uongozi kati ya watoto wa viongozi na wasio wa viongozi waliogombea nafasi hizo ili kuongeza motisha ya vijana kugombea katika uchaguzi ujao.



Ofisa Jinsia wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Zanzibar, Mohamed Jabir akitoa elimu kuhusu madhara ya udhalilishaji wa kijinsia kwa vijana wa kanisa la Anglikani Unguja mwishoni hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Malalamiko mengine yaliyoibuka baada ya watoto hao kutangazwa washindi yalikuwa ni kuhusu umri wa

wa watoto hao katika kutimiza majukumu yao ya kiuongozi ikizingatiwa wanaowaongoza wapo waliowazidi umri.

Mmoja wa waliokosoa alikuwa ni mtoto wa hayati baba wa Taifa, Julius Nyerere, Madaraka Nyerere, kwa hoja kuwa umri wa watoto hao bado ni mdogo kujihusisha na siasa na kushauri waachwe mpaka watakapofikia umri wa kupiga kura.

Katika uchaguzi huo, uliofanyika Desemba 20, mwaka huu, baadhi ya walioibuka kidedea ni mtoto wa msanii wa Bongo Fleva (Shetta), Qailah Nurdin Bilal, aliyechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chipukizi Taifa katika Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mwingine ni mtoto wa Waziri wa Ardhi, Simba Jerry Silla, aliyechaguliwa kuwa Mjumbe wa Chipukizi katika kamati ya uendeshaji taifa upande wa wavulana huku kwa wanawake alishinda Briana Mahiga.

Nafasi ya Mjumbe wa Chipukizi Baraza Kuu la UVCCM ilichukuliwa na mtoto wa Waziri wa Fedha (Dk. Mwigulu), Isack Nchemba wakati Zanzibar ilichukuliwa na Amina Mohammed.



# Jongowe: Kijiji cha kisiwani kisicho na huduma za uzazi

## -Mkunga wa jadi asimulia kupoteza pacha watatu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NI mwendo wa dakika 20 kwa boti kutoka Bandari ya Mkokotoni hadi Kisiwa cha Tumbatu, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Shughuli kuu za wenyeji wa kisiwa hicho ni uvuvi na kilimo cha choroko, mbaazi na mahindi.

Kisiwa hicho ambacho ni miongoni mwa visiwa vidogo 10 vinavyokaliwa na watu wa Zanzibar, kina vijiji vinne vya Jongowe, Gomani, Uvuvini na Mtakuja. Kila kijiji kina sheha wake, shule na zahanati, lakini baadhi ya vituo hivyo vya afya, havitoi huduma ya uzazi.

Mathalani, kijijini Jongowe, zahanati yao inatoa huduma kwa wagonjwa wa nje pekee zinazotolewa mchana kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi 9:30 alasiri kila siku.

Kwa mujibu wa Katibu Tawala Wilaya ndogo ya Tumbatu, Khatib Habibu, Zahanati ya Jongowe ina watumishi saba. Kati yao, waaguzi ni wawili na watano ni wafanyausafi ambao kutokana na uhaba wa watumishi uliopo, wanatwikwa majukumu ya nesi.



Zahanati ya Jongowe Zanzibar **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

Zahanati hiyo kutotoa huduma za uzazi kumewalazimu wenyeji kukimbilia kwa wakunga wa jadi kupatiwa huduma, jambo ambalo ni kinyume cha maelekezo ya kisera katika kukabiliana na vifo vitokanavyo na uzazi nchini.

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Kijiji cha Jongowe kina wakazi 3,821 (wanawake 2,009 na wanaume 1,812), sawa na asilimia 32 ya wakazi wote 11,955 wa Kisiwa cha Tumbatu.

Mtumwa Ngwali Haji (50), mama wa watoto saba, anasema watoto wake wote alijifungua chini ya uangalizi wa wakunga wa jadi kutokana na kijiji chao kutokuwa na kituo cha afya kinachotoa huduma ya uzazi.

"Huduma za kujifungua hazipatikani kijijini hapa, lazima usafiri kwa boti hadi kijiji jirani cha Uvuvini ambako kutokana na jiografia ya kisiwa, ni vigumu kwa mjamzito kukifikia kwa haraka.

"Ukiamua kutembea kwa mguu ni mwendo wa kilomita tisa kuifikia Zahanati ya Uvuvini na unakatisha msitu mkubwa," anasema Mtumwa.

Jabu Makame (42), mama wa watoto watano ana simulizi kama ya mtangulizi wake Mtumwa. Anasema watoto wanne amejifungua chini ya uangalizi wa mkunga wa jadi, lakini alilazimika kupelekwa Hospitali ya Wilaya (Kivunge) wakati wa kujifungua mtoto wake wa mwisho mwaka juzi baada kubainika alihitaji upasuaji.

"Mimba inapokuwa na tatizo tunapewa taarifa tukajifungue hospitalini, hivyo tunalazimika kuondoka hapa kijijini kabla ya mimba haijafika muda wa kujifungua.

"Inabidi utoke mapema huku kwa sababu kwa mila na desturi zetu huku, ni mwiko kuondoka kijijini mimba ikiwa karibu kujifungua," anasema Jabu.

Anasema wanatambua kujifungua kwa wakunga wa jadi ni hatari, lakini hawana chaguo lingine kwa sababu hakuna kituo cha afya kinachotoa huduma ya uzazi kijijini kwao.

"Zahanati yetu ya Jongowe inatoa huduma za msingi tu kama kupima ukuaji wa mimba, wingi wa damu na chanjo kwa mjamzito na mtoto mchanga," anafafanua Jabu.

Tumu Silima Bakari (40), mama wa watoto watano na mkazi wa kijiji hicho, anakitaja kituo chao hakina msaada mkubwa kwa wajawazito kwa kuwa hakina huduma ya uzazi. Anasema zahanati hiyo si tu haina wodi kwa ajili ya uzazi, bali pia haina wataalamu wa kutoa huduma hiyo.

"Tunahitaji wataalamu ili kuokoa maisha yetu na watoto hasa wakati wa kujifungua," mama huyo anawasilisha kilio chao.

### WAKUNGA WALONGA

Salma Haji Ali (54), mmoja wa wakunga wa jadi kijijini Jongowe, anabainisha kuwa kwa miongo miwili sasa amekuwa anatoa huduma za uzazi kijijini huko na ameshahudumia zaidi ya wajawazito 50.

"Ujuzi huu sikusomea popote, bali nilijifunza toka kwa mama yangu mzazi ambaye pia alikuwa mkunga maarufu katika kijiji chetu na aliwasaidia wajawazito wengi. Nilianza kutoa huduma hii nikiwa na umri wa miaka 34. Ninawasaidia tu, hakuna malipo yoyote.

"Lengo langu ni kuokoa maisha ya wanawake na watoto. Sifanyi kazi ili kujipatia ujira. Ninafanya kwa kubahatisha maana sina uwezo wa kuzuia madhara yanayoweza kutokea, ikiwamo kifo.

"Mara chache huwa ninapewa chochote, lakini siombi malipo maana kama nilivyokueleza awali, ninafanya kazi hii ili kuokoa maisha ya wanawake wenzangu na watoto," anafafanua.

Mkunga Salma anabainisha kuwa kwa mwezi, huzalisha wastani wa wajawazito watano.

"Ni kazi ngumu yenye changamoto, lakini ninaifanya kwa ujasiri na moyo wa huruma, mara nyingine wajawazito wanaokuja hawakupi taarifa sahihi kuhusu maendeleo ya ujauzito," anasema.

Anakumbuka jinsi alivyokumbana na changamoto ya kumzalisha mjamzito aliyekuwa na watoto pacha watatu bila kutambua idadi ya watoto tumboni.

"Alipokuja nilidhani alikuwa na mtoto mmoja. Baada ya kumzalisha mtoto wa kwanza, aliendelea kujifungua wa pili na baadaye wa tatu. Bahati mbaya wote watatu walipoteza maisha," Salma anasimulia tukio hilo kwa upole huku uso wake ukikosa tabasamu.

Changamoto nyingine, Salma anaitaja ni kutokuwa na vifaa vya kutolea huduma ya uzazi mipira maalum ya kutandika, hivyo kulazimika kutumia kanga.

"Wakati mwingine anakuja mjamzito tayari muda wa kujifungua umewadia, lakini hana zana yoyote, hivyo ninatumia kanga kumsaidia. "Wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu, ninachukua tahadhari kujikinga na maradhi ya kuambukiza.

"Ninamshukuru Mungu katika kipindi cha miongo mitatu, hakuna mjamzito aliyepoteza maisha mikononi mwangu," anahitimisha mkunga huyo.

### WADAU, SERIKALI

Rajab Khamis Rajab, Mratibu wa Huduma za Afya Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, anasema kijiji cha Jongowe kina zahanati inayotoa huduma za ngazi ya msingi, akikiri haina sifa ya kutoa huduma ya uzazi kutokana na kutokuwa na miundombinu na wataalamu wenye sifa ya kutoa huduma hiyo.

"Ikishakuwa na miundombinu na wataalamu wenye sifa hiyo, zahanati hiyo inaweza kupandishwa daraja na kutoa huduma ya uzazi, lakini lazima pia ijengwe nyumba ya madaktari," Rajab anasema.

Kwa mujibu wa mratibu huyo, kwa sasa zahanati hiyo haina nyumba kwa ajili ya watumishi. Muuguzi mmoja amepanga kijijini na mwingine anaishi mjini Unguja, husafiri kila siku kwenda kutoa huduma. Wafanyausafi ni wakazi wa kijiji hicho.

Mwandishi aliyefunga safiri hadi kijijini Jongowe, alibaini kuwa nauli ya kutoka Bandari ya Mkokotoni hadi Kisiwa cha Tumbatu ni Sh. 1,500 kwa boti inayofanya safari kila siku kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 10:00 jioni. Katika dharura, boti hiyo hukodiwa kwa Sh. 25,000.

Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar) hakiko mbali na yanayojiri kisiwani Tumbatu.

Mratibu wake wa Mradi wa Afya ya Uzazi, Zaina Abdalla Mzee, anasema huduma ya afya ya uzazi katika Kijiji cha Jongowe zinahitajika ili kuokoa maisha ya mama na mtoto.

"Tulifanya utafiti na kubaini huduma za afya ya uzazi bado zina changamoto ikiwamo Kijiji hicho cha Jongowe. Tulibaini wazazi wanaamini wakunga wa jadi kwa sababu eneo lao halina wataalamu wa afya ya uzazi," anasema.

Katibu Tawala Wilaya ndogo ya Tumbatu, Khatib Habibu, anakiri Kijiji cha Jongowe kinakabiliwa na tatizo la kukosa huduma ya uzazi kwa wajawazito.

"Jongowe hakuna miundombinu kwa ajili ya huduma za uzazi, hivyo wajawazito wanalazimika kujifungua nyumbani na wache wanakimbilia Hospitali ya Kivunge (Hospitali ya Wilaya) hasa wale wenye matatizo ya afya ya uzazi," anasema.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, kwa kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023, vifo vitokanavyo na uzazi Zanzibar viliripotiwa kwa kinamama 46 na watoto wachanga wenye umri chini ya siku saba 1,567.

Wizara hiyo pia inabainisha kuwa katika kipindi hicho, wajawazito 38,097 (Unguja 26,405 na Pemba 11,692) walijifungulia hospitalini na vituo vya afya.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, anasema licha ya changamoto ya kutokuwa na miundombinu ya huduma za uzazi katika baadhi ya vijiji, idadi ya wajawazito wanaojifungulia hospitalini na vituo vya afya imeongezeka kulinganishwa na miaka ya nyuma.

Mazrui anasema mwaka wa fedha 2022/23, wajawazito 52,891 walihudhuria kliniki angalau mara moja katika kipindi cha ujauzito. Kati yao, 9,017 (sawa na asilimia 17) walihudhuria kliniki wakiwa na ujauzito chini ya wiki 12 na kwamba serikali inatarajia kujenga hospitali ya kisasa itakayotoa huduma za dharura kwa wajawazito katika Kisiwa cha Tumbatu.

Anasema hospitali hiyo itapunguza tatizo la wajawazito kujifungulia kwa wakunga wa jadi na kuvuka bahari kwa lengo la kupata huduma katika Hospitali ya Wilaya (Kivunge).

Waziri Mazrui anasema kuwa kwa mwaka huu wa fedha (2023/24), serikali imetenga Sh. bilioni 189.3 kwa ajili ya sekta ya afya.

# KRISMASI PICHANI



Kupanda farasi katika ufukwe wa Coco ni Sh.3000 ukitembezwa utalipia Sh.5000, katika kipindi cha Sikukuu ya Krismasi.



Wananchi wakiogelea katika ufukwe wa Coco jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya kusherehekea Sikukuu ya Krismasi. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**



Paroko wa Parokia ya Mtakatifu Petro Oysterbay, Padri Alister Makubi, akiongoza ibada ya ubatizo iliyofanyika katika kanisa hilo jijini Dar es Salaam jana.



Paroko Msaidizi wa Parokia ya Mtakatifu Petro Oysterbay, Padri Chinnadurai Selvaraj ( kushoto), akimpaka mafuta ya Krismasi mtoto Evelyne Joseph, wakati wa ibada ya ubatizo iliyofanyika katika kanisa hilo jijini Dar es Salaam jana.



Baadhi ya wananchi waliofika fukwe za bahari ya Hindi kufurahi kipindi cha Sikukuu ya Krismasi, katika eneo la Coco jijini Dar es Salaam jana.



Wazazi wakiwa na familia zao wakipumzika katika fukwe za bahari ya Hindi eneo la Coco jijini Dar es Salaam jana, kipindi cha Sikukuu ya Krismasi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# NHIF, wamiliki wa hospitali binafsi wamalize jambo hili

**WAMILIKI** wa hospitali binafsi nchini, wametishia kugoma kupokea wagonjwa wanaohudumiwa kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa kile walichodai ni hatua ya kupinga gharama mpya za huduma zilizotolewa na mfuko huo. Hali hiyo inatokana na hivi karibuni NHIF kupunguza baadhi ya gharama zitakazoanza kutumika Januari Mosi, mwakani.

Sababu kubwa wanayoitoa wamiliki hao wa hospitali binafsi ni kwamba kitita kipya kilichotangazwa na taasisi hiyo yenye dhamana ya kutoa unafuu katika matibabu, kinaweza kusababisha hasara kwao na kuna uwezekano wa baadhi ya hospitali kufungwa kutokana na hasara watakazopata. Wanabainisha kuwa miongoni mwa gharama zilizoshushwa ni kumwona daktari, upasuaji na kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo.

Aidha, wamiliki hao wanasema takribani miaka saba iliyopita, gharama zinazotumika sasa zilipotangazwa, hakuna maboresho yoyote yaliyofanyika na kwamba walitarajia NHIF ingeongeza gharama katika kitita kilichotangazwa lakini mambo yaliyofanyika ni kinyume cha matarajio. Pia wameeleza kutokushirikishwa katika upangaji wa gharama jambo ambalo linaonekana kama wanaburuzwa na wanapaswa kutekeleza uamuzi uliofanywa.

Katika kujenga hoja yao kuonekana ni halali, wamiliki hao wameweka hadharani kwamba mfuko huo umekuwa ukichelewesha malipo hata kwa miezi sita na wakati mwingine kukataa baadhi ya madai na kwamba kumekuwa na mfumuko wa bei, kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Kitanzania dhidi ya Dola ya Marekani kwa asilimia 20 ndani ya miaka saba. Kwa sababu hizo na zingine, wamesema itawawia vigumu kutoa huduma kwa wanachama wa NHIF.

Hatua iliyochukuliwa na NHIF kupunguza gharama hizo katika kitita cha huduma za matibabu zinatoa unafuu kwa wagonjwa lakini kwa upande mwingine ni maumivu kwa watoa huduma. Hata hivyo, katika mtazamo yakinifu, kama wanavyodai watoa huduma hao, hatua hiyo inaweza kuwa maumivu kwa wagonjwa kwa sababu iwapo hospitali binafsi zitagoma kupokea wagonjwa wanaotumia huduma ya NHIF, kutakuwa na mlolongo mkubwa kwa hospitali za umma kuliko ilivyo sasa.


Kama inavyoeleweka, katika hospitali nyingi za umma kuanzia zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya, kwenye madirisha ya bima ya afya kumekuwa na misururu ya wagonjwa ambao wakati mwingine huchelewa kupata huduma. Hata katika baadhi ya hospitali kama Aga Khan kwenye vituo vya kutolea huduma pembezoni kama Tabata, kumekuwa na foleni kubwa ya wagonjwa. Swali la kujiuliza ni je, kama kutatokea mgomo wa hospitali binafsi kuwakataa wanachama wa NHIF hali itakuwaje.

Jambo lingine linalopaswa kuzingatiwa ni kwamba huduma katika hospitali za umma hazitolewi kwa viwango stahiki licha ya kwamba baadhi ya viongozi wamekuwa wakisema zimeboreshwa lakini kiuhalisia kuna changamoto nyingi. Suala hili, hakika kama halitatiliwa mkazo, linaweza kusababisha athari kwa wagonjwa.

Kama mwanafalsafa wa zamani wa dola ya Ugiriki, Socrates, alivyowahi kusema wapiganapo tembo ni nyasi ndizo ziumiazo, ndivyo inavyoweza kutokea kwa wagonjwa kuathirika iwapo jambo hili halitapatiwa ufumbuzi. Kama mambo mengi yanafanyika kwa njia shirikishi, kwa nini hili la kupanga gharama mpya halikufanyika kwa njia hiyo?

NHIF inapaswa kukutana na wadau na watoa huduma za afya, hususan wamiliki wa hospitali binafsi na ili kulitatua jambo hili kabla ya wagonjwa kupata madhara. Katika jambo hili, katu kusiwapo kutunishiana misuli bali kuwe na maelewano ya pande zote katika kuleta afya na tija kwa wagonjwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Waliokwama kimasomo wawe na ari mpya 2023

Na Mwandishi Wetu

**MSISITIZO** wa serikali mtoto wa kike apatiwe elimu hata kama alikatisha masomo hapo awali ni kauli mbiu inayopaswa kugusa familia na mabinti wenye changamoto za kielimu wanapoanza mwaka 2023.

Kwa kutambua mambo mengi yanayowakwamisha wasichana kusoma kama kubakwa na kupata ujauzito, kuozwa utotoni, kuugua, kuzuiliwa kusoma na hata kulazimishwa kulea familia , serikali imewaruhusu wasome bila kuangalia kuwa walianguka.

Ndiyo wakati wa kutimiza msemo kuwa ukimwelimisha mtoto wa kike, umeelimisha jamii nzima, ni kwa sababu mwanamke anabeba majukumu makubwa ndani ya familia na taifa kuanzia uzazi hadi kulea.

Wadau wasaidie juhudi za serikali ili wasichana wapate haki zao za msingi ikiwamo elimu, baada ya kutambua kuwa watoto wa kike wana changamoto za kipekee wanazokutana nazo kila siku.

Ni lazima kuhimiza utoaji haki sawa ili kupata elimu kwa watoto wa jinsi zote na mtoto wa kike waelimishwe na kupatiwa huduma stahiki ili waweze kutambua haki zake na hivyo kuifanya Tanzania kuwa mahali bora pa kuishi kwa ajili yake na taifa pia.

Serikali inatekeleza mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala (SEQUIP), ambao pamoja na mambo mengine utampa fursa a elimu msichana aliyekwamishwa kimasomo.

Lengo ni kuwafikia wasichana 12,000 nchi nzima wenye umri wa kati ya miaka 13 hadi 21 katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2022.

Juhudi za kuwafundishe ziwape moyo pengine walioko mbali na vituo vya kusomea , waandaliwe utaratibu wa kujisomea mwenyewe nyumbani, huku juhudi za kupata mabweni zikiendelea.

Wakati hayo yakifanyika kuna vitu vinavyokwamisha wasichana kusoma mfano ukosefu wa pedi hasa wanaoishi vijijini, hilo nalo liangaliwe .

Serikali ione umuhimu wa kuondoa kodi kwenye pedi ili ziwafikie wasichana wanaoteseka kwa kukosa bidhaa hizo muhimu kila mwezi na hata kulazimika kuacha shule.

Hata hivyo , taifa lianzishe utaratibu wa ubunifu unaowawezesha watafiti kubuni na kuibua aina mbalimbali za pedi bora ambazo zitawasaidia wasichana kwenye tatizo hilo ambalo ni changamoto kubwa licha ya kupuuzwa.

Ipo teknolojia ya kutengeneza pedi ambayo inatumiwa dunia nzima , ni vyema kuliangalia suala hilo na ikibidi kuhaulisha teknolojia na kuwasaidia wasichana wasikwame maana pedi ni sehemu ya huduma zinazohitaji kwenye kufikia afya bora ya uzazi na usikivu darasani.

Masomo ya stadi za maisha yalete ubunifu wa kupata taulo bora na mbadala kwa wasichana maelfu wa taifa hili na wajengewe uwezo wa kuzizalisha .

Leo, suala la hedhi linaendelea kuwa kama mwiko kwenye jamii. Inazihusisha na aibu, jamii inachukulia hali hiyo kama jambo la kificho linalofaa kuwa siri ya mwanamke.

Ukweli sivyo. Ni michakato ya uzazi na maumbile. Ni wakati wa shule kufundisha na kueleza wanafunzi kuanzia wavulana na wasichana kuwa si kitu cha aibu na kuwaelimisha kuwa ni masuala ya kawaida ili kuondoa unyanyapaa.

Uelimishaji jamii kuhusu hedhi salama hasa shuleni utatokomeza mazoea ya kuwanyanyapaa, kuwakejeli wasichana shuleni hasa wale wanaoonekana kuwa wamepevuka na kuanza hedhi.

Juhudi za kuwarejesha wasichana hao shuleni zikienda sambamba na kuelimisha jamii kuhusu habari za kukua na mabadiliko ya kimwili ya watoto wa kike yalenge kupunguza unyanyapaa.

Ni wazi kuwa wasichana waliopata mimba wanaporejea kwenye masomo mitaani hata shuleni wanakutana na unyanyapaa kwa vile wanaonekana kama wameshakuwa wakubwa na wanaojihusisha na masuala ya mahusiano.

Iwapo jamii itapata uelewa kuhusu michakato hiyo mambo hayo yataondoka na dharau, kejeli pamoja na dhihaka kwa wasichana zitakoma.

Ifahamike kuwa kumwelimisha mwanamke ni kuelimisha taifa na kumwekea mazingira wezeshi ili asome ni kuongeza thamani katika maisha yake na ya taifa.

# Akutwa amejinyonga chumbani kwa chandarua mkesha Krismasi

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Mtaa wa Ronsoti, kata ya Nyamisangura katika Halmashauri ya Mji Tarime, Charles Bwanga, amekutwa amejinyonga hadi kufa chumbani kwake kwa kutumia chandarua wakati wa usiku wa Sikukuu ya Krismasi.

Imedaiwa na majirani kuwa huenda Bwanga ambaye ni maarufu mjini hapa, amefikia hatua hiyo ya kukatisha uhai kutokana na msongo wa mawazo baada ya kukimbiwa na mke na Watoto.

Diwani wa Nyamisangura, Thobias Ghati, na mwenyekiti wa zamani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mara, Samwel Kiboye, walieleza kusikitishwa na kifo cha Bwanga ambaye alikuwa maarufu mjini hapa.

"Tumesikitishwa na kifo cha kujinyoga cha mkazi wa mtaa wetu huu wa Ronsoti. Inawezekana huenda alikumbwa na msongo wa mawazo baada ya kukimbiwa na mke pamoja na watoto na kwenda kuishi mbali na yeye na kubaki mwenyewe

Kifo hiki kimeleta majonzi katika mtaa wao na kata ya Nyamisangura. Tunatoa wito kwa jamii wanapokuwa na migogoro ya kifamilia, wajaribu kuwashirikisha ndugu wa karibu na viongozi wa serikali ili kutatua na kuishi kwa amani, kutunza familia kwa ajili ya maendeleo ya familia na taifa badala ya kujichukulia sheria mkononi ikiwamo uamuzi mgumu kama wa kujitoa uhai. Jambo hili kwa Mwenyezi Mungu halikubaliki," alisema.

Kiboye, maarufu kama Namba Tatu, alisema: "Tunasikitika sana wakazi wa Ronsoti kwa tukio hili la Bwanga kujinyonga nyumbani kwake. Mbali na kukimbiwa na mke na watoto, asingechukua uamuzi mgumu wa kujitoa uhai kwani wanawake kutoroka na kwenda na watoto si jambo geni.

"Nadhani suala hili lingeweza kusuluhishwa na kurejea pamoja na kuishi kama kawaida na familia yake. Hili la kujitoa uhai ni kitendo ambacho kinatakiwa kulaaniwa na jamii kujiepusha na kujichukulia sheria mkononi."

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tarime Rorya, Kamishna Msaidizi (ACP) Michael Njera, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwataka wananchi kutojichukulia sheria mkononi na kujitoa uhai.

Aidha, alitoa wito kwa jamii kama kuna mgogoro wa kifamilia, ni bora kufikisha kwa ndugu na jamaa wa karibu na hata uongozi wa serikali ili kusuluhisha badala ya kujitoa uhai.

Kamanda Njera alisema mwili wa Bwanga umehifadhiwa katika chumba cha maiti cha Hospitali ya Wilaya Tarime kwa uchuguzi zaidi.



Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Ramadhan Ng'azi (kushoto), akishuhudia dereva wa basi akipimwa kiwango cha ulevi katika kituo cha mabasi mjini Songea mkoani Ruvuma juzi, ikiwa ni mwendelezo wa kamanda huyo wa kukabiliana na ajali nchini, wakati huu wa kuelekea mwisho wa mwaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watanzania wasomi watakiwa kuacha kasumba kupenda vya nje

**Na Vincent Mpepo,** OUT

WATANZANIA wasomi wametakiwa kuacha kasumba ya kupenda vitu, bidhaa na programu za vyombo vya habari kutoka nje ya nchi na kuwa wazalendo kwa kupenda vya ndani ikibidi kupitia taaluma na ujuzi wao wasaidie kuboresha.

Ushauri huo ulitolewa na Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dk. Athuman Samzugi, wakati akifungua mafunzo ya siku mbili ya vigezo vya kutathimini habari yaliyofanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuria na wahadhiri wa tasnia ya habari kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC) na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Alisema wakati umefika kwa waafrika na hususani wasomi kupenda vitu vyao badala ya kupenda kila kitokacho nje ya nchi kitu ambacho sio uzalendo na kinafifisha juhudi za maboresho ya kufanya vitu hivyo viwe na ubora na vya kukubalika kitaifa na kimataifa.

"Kwa nini habari za Afrika haziandikwi na waafrika wenyewe?" Alihoji Dk. Samzugi.

Alisema mtizamo wa maudhui ya Afrika unaripotiwa na wageni kwa matukio hasi kitu kinachotia shaka na doa kuhusu uzuri wa historia njema ya Afrika na kwa mtizamo huo hasi unaonesha kuwa ni bara la shida, matatizo na majanga wakati uhalisia haupo hivyo.

"Matokeo yake tunatenegeza kizazi cha wanajamii ambao ni watanzania kwa asili, lakini wana utamaduni na maadili yasiyo ya kitanzania na kiafrika," alisema Dk. Samzugi.

Alisema wananchi wamekuwa walaji wa habari kutoka nje na kudharau habari za ndani na wasomi ndio wanaoongoza kwa kasumba hiyo.

Alisema hali hiyo inakuza na kulea kizazi cha watu ambao hawaujui utamaduni wao na kujua tamaduni za kigeni kama vilewa Kichina, Kikorea au Kifilipino kupitia tamthilia na programu nyingine za redio na runinga kutoka nje.

Alisema kama Watanzania wasipoandika habari zao wenyewe wataandika kwa namna wanavyopenda wao kitu ambacho siyo sawa.

Aidha, alisema msomi anasema hawawezi kuangalia kituo cha habari cha ndani na kuhoji "je ni kweli kuwa maudhui yetu hayakidhi mahitaji ya wasomi na jamii zetu?"

Mtafiti kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Abdallah Katunzi, alisema bado kuna changamoto ya ufinyu wa maudhui katika vyombo vya habari katika runinga na redio.

"Matokeo yake ni kuwa na maudhui yasiyo na tija kwa umma katika vyombo vya habari huku sehemu kubwa ya muda ukitumika katika burudani na michezo," alisema Katunzi.

Mhadhiri Msaidizi kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Kahenga Dachi, alisema mafunzo hayo yamewasaidia kupima na kutathmini ubora wa habari kwa vigezo ambavyo vimefanyiwa utafiti.

"Tunatakiwa kuwa na waandishi wa habari ambao wataandika habari zitakazosaidia wananchi kuwa na mawanda mapana ya habari ili waweze kufanya maamuzi sahihi," alisema Dachi.

Vile vile, alisema waandishi wa habari hawapembui waandikacho na huchapisha habari ambazo hazina usuli na historia ya vyanzo halisi vya matatizo na changamoto za jamii kitu ambacho kinashusha hadhi ya taaluma ya uandishi wa habari.

Mhadhiri kutoka Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Malima Zacharia, alisema mapendekezo na makubaliano ya mijadala katika mafunzo hayo yatafanyiwa kazi na shule yake ipo tayari kutoa ushirikiano kwa wahadhiri wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ili kuhakikisha maudhui hayo yanaingizwa kwenye mitaala ya shahada za awali na umahiri.

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed






Maofisa waandamizi wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), akiwemo Ofisa Uhifadhi Mkuu wa Hifadhi hiyo, Gladys Ngu'umbi (wa pili kushoto) wakiwapongeza baadhi ya wafanyakazi wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) na wadau wa utalii mkoani Kilimanjaro wakiwemo waandishi wa habari muda mfupi baada ya kurejea kutoka safari ya kihistoria ya kupanda Mlima huo kwa lengo la kufikisha mashine ya kufanyia miamala (POS Machine) ya benki hiyo kileleni ili kusogeza huduma za benki hiyo kwa wateja wake wanaotembelea mlima huo. **PICHA: KINAPA**

# Watalii kupata huduma miamala kifedha kilele Mlima Kilimanjaro

**Na Halfani Chusi**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imepeleka mashine ya kufanyia miamala (POS Machine) katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, itakayowawezesha watalii kupata huduma za kifedha wakiwa mlimani.

Lengo lingine wamelitaja ni kudhihirisha ubora na ufanisi wa mashine hiyo ya miamala katika utoaji wa huduma kwenye mazingira yoyote yakiwamo yenye miinuko mikubwa.

Ofisa Uhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA), Gladys Ngu'umbi, aliyasema hayo katika hafla ya kupokea wafanyakazi waliopanda mlima huo, Desemba 16, mwaka huu, kupeleka huduma hiyo.

Hafla hiyo ilifanyika mwishoni mwa wiki katika geti la lango la Marangu ikihudhuriwa na Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru, wafanyakazi wa benki hiyo na baadhi ya wadau wa utalii pamoja na wateja.

Ngu'umbi aliipongeza benki hiyo kwa kuutumia mlima huo kama kigezo cha kuthibitisha ubora na ufanisi wa mashine hiyo ya miamala pamoja na kusogeza huduma zao katika kivutio hicho cha kimataifa.

Alisema hatua hiyo itasaidia kurahisisha malipo mbalimbali yanayofanywa na wageni wanaotembelea hifadhini.

"Kwetu sisi kama wadau wa utalii, ujio wa huduma hii ni mkombozi dhidi ya changamoto ya huduma ya malipo iliyokuwa ikiwakabili wadau mbalimbali hususani wasindikiza wageni.

"Baadhi yao walikuwa wanalazimika kuwafuata watalii hadi nje ya hifadhi huko ili tu kufuata malipo yao. Kupitia mashine hii, malipo yanaweza kufanyika huko kileleni wakiwa wanajipongeza," alibainisha Ngu'umbi kauli ambayo iliungwa mkono na Hillary Kombe na Godlisten Mkonyi wanaotoa huduma za kusindikiza wageni katika mlima huo.

Mkurugenzi wa Biashara wa NBC, Elvis Ndunguru, alisema hatua hiyo imelenga kuunga mkono jitihada za serikali katika kukuza utalii wa ndani na nje kwa kuutangaza mlima huo.

"Tuna tabasamu siyo tu kama washindi ila kwa kumshukuru Mungu kwa kutupa usalama na afya kufanikisha zoezi la kufikisha tabasamu hadi kilele cha Mlima Kilimanjaro, ambapo POS za NBC sio tu zimefika kilele cha Mlima Kilimanjaro bali pia, zimewaka na kufanya miamala.

"Tunajivunia kuwa waanzilishi wa uzinduzi wa kwanza wa mashine ya POS katika kilele cha Mlima Kilimanjaro zimeweza kufanya miamala katika vituo vyote, Mandara, Horombo, Kibo, Gilmans Point, Stella na hadi Uhuru Kileleni.

"Hii ni kuwahakikishia wateja wetu kuwa, mashine hizi ni imara za uhakika na zinafanya kazi wakati wowote, kwenye mazingira yoyote na hali ya hewa yoyote," alisifu Ndunguru alisisitiza kuwa, sababu ya kuzindulia mashine hiyo kwenye mlima huo inatokana na sifa kuu tano zinazoendana na alama na maana ya vituo wanavyokutana navyo katika kupanda Mlima Kilimanjaro.

Alisema wanaamini kila kituo kimeoana na sifa za mashine zao zenye urahisi, haraka au kasi, teknolojia ya hali ya juu, mahiri (Smart) na uhuru wa malipo.

Alisema jitihada hizo ni muendelezo wa kampeni yao mpya ya 'Tabasamu Tukupe Mashavu,' ya benki hiyo inayolenga kutoa fursa kwa wateja kufurahia pamoja na wapendwa wao katika sikukuu za mwisho wa mwaka kupitia miamala iliyorahishwa kupitia benki ya NBC.

Akizungumza kwa niaba ya wafanyakazi waliopanda mlima huo, Florence Ng'wavi, alisema mafanikio hayo yanawasilisha adhma ya pamoja ya wafanyakazi wa benki hiyo katika kuthibitisha na kutetea ubora wa huduma wanazozitoa kwa wateja.

# Wadau waomba mikopo iongezwe kuwa 15%

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI sera ya mikopo ya asilimia 10 iliyokuwa ikitolewa na halmashauri nchini ikitarajiwa kurejea tena Januari mwaka ujao, baadhi ya wadau wakiwamo madiwani, wameishauri serikali kuongeza wigo wa kiwango cha sasa hadi kufikia asilimia 15.

Diwani wa Kata ya Kahe iliyoko Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro, Aloyce Mumburi, akizungumza katika kikao cha 12 cha mwaka cha Shirika la Maendeleo ya Jamii (TUSONGE), alisema iwapo Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), itaona kuna ongezeko la makusanyo ya mapato ya ndani katika halmashauri husika, ni vizuri ikaruhusu nyongeza ya kiwango hicho kufanyika.

Aprili 13, mwaka huu, serikali ilisitisha mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na kila halmashauri, ikieleza nia yake ya kujipanga kuweka mfumo mpya wa utoaji wa mikopo hiyo.

Uamuzi huo ulitangazwa Bungeni, Dodoma na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Katika mkutano huo, Mumburi alisema: "Hii mikopo ya asilimia 10. Tunataka iongezeke iwe asilimia 15 ama zaidi. Huko tuendako kama mambo yataendelea kuwa mazuri kwenye makusanyo, TAMISEMI iangalie na ikiwezekana ziongezwe na kuwa asilimia15.

"Kwenye kundi la wenye ulemavu wakapewa tano, na hao wengine wakapewa tano tano zikawa 15, kama itaonekana inafaa kwa miongozo, taratibu na sheria ya mikopo hiyo." Baadhi ya wanufaika wa miradi inayotekelezwa na shirika hilo, Analise Mmari, mkazi wa Kata ya Ivaeny, Wilaya ya Siha, alisema tangu alipojengewa uwezo wa kuhimili mikikimikiki ya maisha ikiwamo kuongeza kipato, amejenga choo cha kisasa.

"Mimi kwa kweli, TUSONGE imenipa manufaa siwezi kueleza. Kwa sababu kwanza hapo mwanzoni nilikuwa sina choo. Ila baada ya kupata elimu ya jinsi ya kuweka akiba, kukusanya fedha yangu kidogo kidogo katika vikundi, na nikaweka hisa yangu, nilipata sifa za kukopa na kwenda kununua mchanga, nikatengeneza choo change bora.

"Mwishoni mwa mwaka huu, nina mpango tena nikivunja kikoba changu, ninakwenda kujenga nyumba yangu ya kisasa. Kweli mimi ninawashauri wanawake ambao hawajajiunga kwenye vikundi vya vikoba na kuweka akiba kwenye taasisi nyingine za fedha wafanye hivyo ili kujiinua kiuchumi."

Imelda Massawe wa Kata ya Biriri, Wilaya ya Siha alisema, "TUSONGE imeninufaisha leo nimeweza kujenga kibanda changu mwenyewe cha biashara, na sasa hivi naendelea vizuri. Ile hali ya aibu kwenda kukopa na kutafuta pesa sina tena kwa sababu nimejengewa uwezo."

Pia, Mary Laizer, mkazi wa Kijiji cha Majengo, alisema, "Nimenufaika sana na mradi wa TUSONGE, tangu ulipoingia kwetu, kwa sababu nimejifunza ujasiriamali, nimejifunza ufugaji, na sasa hivi nafuga kuku 70, nauza kuku, nauza mayai, nasomesha watoto."





# Jumuiya za wazazi zatakiwa kujiimarisha kiuchumi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

KATIBU Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Gilbert Kalima, ameitaka Jumuiya za Wazazi nchini kujiimarisha kiuchumi kwa kuendeleza miradi waliyonayo katika maeneo yao pamoja na kuibua mipya.

Aidha, ameiagiza mikoa ambayo haijaunda kamati ndogo kwa mujibu wa kanuni zanazoongoza jumuiya hiyo, kufanya hivyo mara moja ili zisadie kushughuli mbalimbali za jumuiya hiyo ikiwemo uchumi.

Pia, amewaagiza viongozi wa Jumuiya hiyo katika mikoa yote nchini, kuweka mikakati thabiti ya kusaidia CCM kushinda kwa kishindo katika uchaguzi wa serikali za mitaa, utakaofanyika mwakani pamoja na uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Kalima alisema hayo jijini hapa wakati wa kikao maalum cha Baraza la Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha.

"Hatuwezi kuwa na siasa safi katika jumuiya yetu kama hatutakuwa na uchumi imara, kwa sababu hii ninaziagiza jumuiya za wazazi katika mikoa yote hapa nchini, kuhakikisha wanaiendeleza miradi waliyonayo pamoja na kuibua miradi mipya," alisema.

Aliupongeza Mkoa wa Arusha kwa kuibua miradi mbalimbali ya uchumi, ikiwamo mashine kubwa za kisasa kwa kila wilaya pamoja na mradi wa maduka na pia wanaendelea kuibua miradi mingi zaidi.

"Kipekee nampongeza sana Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Arusha, Hezron Mbise kwa miradi mikubwa ambayo ameanzisha katika Mkoa wa Arusha, lakini pia ametujulisha kabla ya mwaka 2027 atakuwa amefanya jambo kubwa la kihistoria katika Jumuiya hii, ambalo litaisaidia kuwa na uchumi mkubwa," alisema.

Kuhusu kamati ndogo nne zenye majukumu tofauti alizozindua, katibu mkuu huyo ambazo ni Kamati ya Elimu, Afya na Mazingira, Habari, Utamaduni na Hamasa, Uchumi, Mipango, Fedha za Uwekezaji na Nidhamu na Maadili, alizitaka kutumia maarifa yao kulingana na majukumu waliyopewa kusaidia jumuiya hiyo, katika masuala mbalimbali ya kiutendaji na kuleta mabadiliko chanya ndani ya jumuiya hiyo hasa uchumi.

"Wajumbe wa kamati ndogo majukumu mliyopewa ni kazi ya kujitolea. Niwaombe mfanye kazi hii kwa moyo kwa kutumia taaluma zenu kuleta maarifa, ubunifu katika kuisadia jumuiya yetu kufanya vizuri zaidi tofauti na hivi sasa," alisema.

Kalima aliagiza viongozi wa jumuiya hiyo katika mikoa mingine, kuunda kamati hizo mara moja kwa kuwa tangu agizo hilo limetolewa ni Mkoa wa Arusha na Dar es Salaam pekee ndiyo imekamilisha maadalizi ya kamati hizo.

Kuhusu uchaguzi wa serikali za mitaa, Kalima aliwataka wanachama wa Jumuiya hiyo, kuisadia CCM kupata ushindi wa kishindo ambao utaakisi ushindi wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

"Chama cha siasa bila kushika dola ni ubabaishaji. Hivyo lazima tuhakikishe CCM inaendelea kushika dola kwa sisi kuwa kisemeo cha wananchi kwenye serikali ili zifanyiwe kazi wananchi waneдelee kutuamini wakipigie kura chama chetu," alisema.

Awali, akifungua kikao hicho cha Baraza Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Mkoa wa Arusha, Mbise alisema katika kipindi cha uongozi wake, atahakikisha jumuiya hiyo inajikwamua kiuchumi kwa kumiliki miradi mbalimbali.



Katibu Tawala wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, kulia akiteta jambo na Mbunge wa jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma juzi katika kikao cha kawaida cha Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya, kilichofanyika kwenye ukumbi wa Tate Plus kilichojadili utekelezwaji wa ilani kuanzia mwezi Januari hadi Desemba mwaka 2023. **PICHA:STEVEN WILLIAM**

# Mbunge Muheza aridhishwa utekelezaji miradi

**Na Steven William,** MUHEZA

MBUNGE wa Jimbo la Muheza, Hamisi Mwinjuma amesema anaridhishwa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Wilaya ya Muheza.

Alisema hayo katika kikao cha kawaida cha Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) wilaya, kilichofanyika kujadili utekelezwaji wa ilani kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2023.

Mwinjuma ambaye ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, alisema anajisikia furaha kuona watendaji wa serikali wilayani Muheza wanavyomwakilisha vyema Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan katika kutekeleza ilani ya CCM kwa kusimamia vizuri miradi ya maendeleo.

"Nakiri kuridhishwa kwa namna ilani ya Chama cha Mapinduzi inavyotekelezwa kwa ukamilifu na najisikia furaha kuona watendaji wa serikali wilayani Muheza wanavyomwakilisha vyema Rais," alisema Mwana FA. Aliwaomba wajumbe katika mkutano huo hususani wanawake kumpa kura zote za ndiyo Rais Samia katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki akiwasilisha taarifa ya serikali ya miradi ya maendeleo, alisema wanamshukuru Rais Samia kwa kutoa fedha nyingi za miradi zaidi ya Sh. bilioni 10.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Dk. Jumaa Mhina, alisema katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza wanatekeleza miradi mbalimbali ikiwamo ya afya, utawala, maji, elimu na miradi mingine. Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza, Erasto Mhina, alimshukuru Rais Samia kwa kuijali wilaya ya Muheza kutoa fedha za miradi na kuahidi kuisimamia kuikamilika haraka na ubora zaidi.

Katibu wa CCM wilaya ya Muheza Simon Leng'ese alisema lengo la CCM ni kusimamia na kufuatilia miradi hiyo ikitelekezwa kama ilivyopangwa.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muheza, Laick Gugu, alisema lazima madiwani wasimamie utekelezaji wa miradi katika kata zao ikamilike haraka na iwe na ubora ili wananchi wafaidike na miradi hiyo.

# Taasisi yatoa zaka kwa wananchi kuonesha shukrani

**Na Steven William,**
MUHEZA

WANANCHI zaidi ya 240 wilayani Muheza, Tanga wamekabidhiwa msaada wa vyakula aina mbalimbali na bahasha za fedha ikiwa kama zaka.

Walengwa wa msaada huo ni wazee, wajane, watu wenye ulemavu pamoja na watu wenye uhitaji.

Msaada huo wa vyakula tani saba umetolewa kwa wananchi na Taasisi ya Silver Crescent kutoka nchini Uturuki katika maeneo ya kijiji cha Majengo, kitongoji cha Mkomani na kijiji cha Kibaranga.

Vyakula vilivyotolewa kwa kila mlengwa ni pamoja na mchele, unga wa sembe, unga wa ngano, maharage, sukari, sabuni na mafuta ya kupikia na fedha katika bahasha kama zaka.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ugawaji wa msaada huo juzi, Mratibu wa Taasisi hiyo Mkoa wa Tanga Omari Shariff, alisema ni moja kati ya miradi wanayoitekeleza kwa Tanzania lengo ni kutoa ushirikiano wa karibu kwa serikali kuwahudumia wananchi kijamii ikiwamo kutekeleza miradi ya kutibu macho bure na uchimbaji wa visima.


Mratibu wa taasisi hiyo nchini, Kadir Komurcu, alisema

msaada huo ni juhudi za taasisi hiyo za utekelezaji wa miradi wanayopatiwa na wahisani na wao kuwafikishia wahitaji kwa wakati. Alisema taasisi hiyo inatekeleza shughuli mbalimbali za kufikisha mahitaji kwa watu wanaokusudiwa hali inayojenga uaminifu kwa wahisani dhidi ya taasisi hiyo.

Alisema kuna zaka na sadaka ambayo hupewa mtu yeyote mwenye uhitaji huku zaka ikitolewa kwa makundi maalum.

Diwani wa Kata ya Majengo wilayani Muheza, Mukadam Sabuni, aliwashukuru wafadhili hao kwa kugawa misaada hiyo ya vyakula na bahasha za fedha kwa wananchi.

Taasisi hiyo pia imechimba visima kadhaa katika Wilaya ya Tanga mjini.





# Wanaoishi na VVU wajitokeza kufanya tohara

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MWITIKIO wa watu wazima kufanya tohara umetajwa kuwa hafifu hali inayosababisha ongezeko la watu wanaojitokeza kupata huduma hiyo wakiwa tayari na maambukizi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi ili kupunguza makali ya virusi.

Hali hiyo inatajwa kusababishwa na dhana potofu iliyojengeka kuwa huduma ya tohara inafanywa bila ganzi, kukaa siku saba bila kufanya kazi yoyote pamoja na kupoteza nguvu za kiume.

Hayo yalibainishwa juzi na Msimamizi wa Kituo cha kutolea huduma za tohara Hospitali ya Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga, Dk. Samson Samweli na kueleza huduma hiyo inavyotolewa kwa vijana kuanzia miaka 15 pamoja na wazee kuanzia miaka 50 bila kubagua.

Alisema, vijana wenye umri wa miaka 15 hadi 19 wanajitokeza kupata huduma kulinganisha na kundi la watu wazima ambao wengi wao wanajitokeza wakiwa tayari na VVU, tundu la uume lakupitisha mkojo kuvuja usaha na wengine ngozi ya juu ya uume kuwa na vindonda akiamini ikitolewa anapona.

Samweli alisema, wanapompokea mteja kwanza wanapima maambuzi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi, wingi wa damu na magonjwa mengine, wale wanaobainika kuwa na VVU wanasajiliwa na kuanzishwa dawa za kufubaza virusi (ARV).

"Baada ya kupewa dawa hizo tunawasubiri kwa muda wa miezi sita ili kushusha kopizi 50 ndipo anarejea na kufanyiwa tohara kwani hatuwezi kumfanyia tohara mteja mwenye VVU," alisema Samweli.

Mratibu wa tohara, Hadji Sued alisema, mwaka uliopita walitarajia kuwapatia huduma wateja 4,526 na kuwafikia wateja 4,000 sawa na asilimia 90 ya malengo yao na kuanzia mwezi Oktoba 2023, wanatarajia kuwafikia wateja 9,186, kulinganisha na malengo ya mkoa, 91,022. Mtoa huduma ya tohara, Linda Kidolezi alisema, inakinga maambukizi ya VVU kwa asilimia 90, magonjwa yanayotokana kwa njia ya mkojo (UTI) na saratani ya kichwa cha uume na mlango wa shingo ya uzazi kwa mwanamke. Wanapopokea mteja wanampatia elimu ya maradhi hayo kabla ya tohara.

# Watahadharishwa umakini watoto msimu wa likizo

**Na Vitus Audax,** MWANZA

KAIMU Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapa, Kamila Labani amewatahadharisha wazazi na walezi kuwa makini na watoto katika kipindi hiki cha likizo ili kudhidhibiti matukio ya moto.

Alitoa tahadhari hiyo jana akizungumza na Nipashe kuhusu udhibiti wa matukio ya moto mwishoni mwa mwaka na kuwataka wazazi kuchukua tahadhara ikiwa ni pamoja na kuweka mbali vifaa vyote vya moto na kufunga vizuri majiko ya gesi. "Watoto wetu ni watundu saana hivyo tuhakikishe viberiti vinawekwa mbali, tukiwaacha nyumbani tuhakikishe majiko ya gesi yamefungwa vizuri hii itasaidia kuendelea kubaki salama," alisema Kamanda Labani.

Kuhusu matukio kwa kabla na baada ya Krismasi, Labani alisema hali ni salama katika mkoa huo.

"Tulipokea taarifa ya mtu kutaka kujirusha kwenye mto wenye maji mengi kwa msongo wa mawazo, lakini tuliwahi na kumwokoa pamoja na kumpa nasaha juu ya kitendo alichotaka kukitekeleza, mengine ni moto mdogo ambao hata hivyo tulikuta wananchi tayari wameudhibiti," alisema.

Aidha alisema hali hiyo ya usalama ni matokeo chanya ya utoaji wa elimu kwa jamii unaofanywa na jeshi hilo mara kwa mara juu ya namna ya kudhibiti na kijinga na moto katika makazi na sehemu za biashara. Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari hivi karibuni Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, aliwatahadharisha wananchi kipindi cha sikukuu kuhakikisha nyumba zinabaki na watu kwaajili ya usalama wao na mali zao.

"Kama mtasafiri au kwenda kwenye sehemu za starehe hakikisheni nyumba inabaki na mtu ambaye anaweza kuwa mwanafamilia au mlinzi anayetoka katika kampuni inayotambulika kisheria hii itasaidia kudhibiti matukio ya wizi," alisema SACP Mutafungwa.

Kuhusu usalama kwa watoto, alipiga marufuku kushiriki katika kumbi za disko za ndani zinazoweza kuhatarisha maisha yao pamoja na maeneo mengine ambayo siyo salama kwa maisha yao.

"Unaweza kuondoka nao hata katika sehemu za fukwe kwa kuhakikisha unakuwa nao wakati wote ili kudhibiti matukio kama yaliyowahi katima maeneo mengine siku kama hizi za sikukuu," alisisitiza.



Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba (kushoto) akizungumza hivi karibuni na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi (hawapo pichani) wakati wa kuhamasisha masuala ya kilimo ili kuongeza tija ya uzalishaji katika msimu wa kilimo mwaka huu. Katikati ni Mkurugenzi wa halmashauri hiyo Justice Kijazi na kulia ni Katibu Tawala Msaidizi Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Singida, Stanslaus Choaji, **PICHA:THOBIAS MWANAKATWE**

# 'Mkataba ujenzi daraja JPM unaendelea kwa kasi'

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Wilaya ya Misungwi, mkoani Mwanza, Paul Chacha, amekanusha uvumi kuhusu mradi wa ujenzi wa daraja la Kigongo-Busisi maarufu kama Daraja la JPM kuwa umekwama na ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 36 kwa mujibu wa mkataba.

Alibainisha hayo juzi katika mahojiano na moja cha chombo cha habari mkoani hapa na kueleza kuwa mkataba wa mradi huo ni miezi 48 sawa na miaka minne.

Alisema kwa mujibu wa mkataba huo unatakiwa kukamilika ndani ya miezi 48 na ujenzi wake unaendelea kwa kasi ukiwa na matumaini ya kukamilika katika muda uliokusudiwa.

"Mkataba huu upo hadi kwenye mitandao hivyo inashangaza kiongozi kuuaminisha umma mambo ya uongo na kusema ulitakiwa kuwa umekamilika jambo ambalo siyo sahihi kwani mradi huu unakamilika rasmi 2024 na ulisainiwa 2020," alisema Chacha.

Kadhalika, utekelezaji wa mradi huo umepitia misukosuko mingi ukiwamo ugonjwa wa uviko-19 ambao uliathiri zaidi nchi ya China ambayo ni watekelezaji wa mradi huo, lakini hakuna siku umesisimama unaendelea usiku na mchana.

"Mpaka mwezi wa tatu 2021 tunapata msiba wa Magufuli mkandarasi alikuwa amepewa malipo ya awali tu Sh. bilioni 87 ikiwa asilimia 24.5 ya ujenzi na mpaka leo fedha zilizolipwa ni zaidi ya Sh. bilioni 400 na daraja lipo asilimia 81 hivyo ninavyosema mwakani litazinduliwa ni kweli," alisisitiza.

Hivi karibuni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ADC Taifa Shabani Itutu, alisema Wilaya ya Misungwi ni moja ya eneo lenye miradi mikubwa ya serikali likiwamo daraja la JPM, lakini utekelezaji wake umekwama na ulitakiwa kukamilika mwaka mmoja uliopita.

Alidai mkataba wa mradi huo ulikuwa ni miezi 36 na mpaka kufikia mwezi wa tatu 2021 daraja hilo lilikuwa asilimia 37 na kutaja kuwa umekwama na ulitakiwa kuwa umekamilika mpaka sasa.

Vilevile, alitaja wilaya hiyo kuwa ina mradi mkubwa wa maji wa Ihelele (KASHWASA) unaosambaza maji katika mikoa ya Shinyanga na Tabora huku eneo hilo likikosa huduma ya majisafi na salama.

Akijibu suala la mradi wa maji kwenda mikoa mingine na siyo wilaya hiyo, alisema mradi huo umetengenezwa kwaajili ya Kahama na Shinyanga na kuongezewa mikoa ya Singida, Dodoma na Tabora na siyo kwaajili ya Misungwi.

"Hata hivyo baada ya kuona mradi huo umeweza kusambaza maji katika maeneo husika na kazi bado inaendelea ulitengenezwa mfumo mwingine kwaajili ya kuhudumia vijiji zaidi ya 33 katika Kata za Shilalo na Mbalika hapahapa Misungwi," alisisitiza Chacha.

Kwa heri 2023 ulijaa yaliyoshangaza, ukiondoka na Watanzania 80 Hanang'



Ukurasa 13



Ukurasa 14

## Diwani asiyeona anayeteswa na uduni wa miundombinu

siasa
JUMATANO DESEMBA 27, 2023
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# 2023 ulivyomuweka Rais Samia kileleni kiumaarufu kisiasa

**Na Ani Jozeni**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anapoelekea kutimiza miaka mitatu uongozini, mwaka 2023 umempa mafanikio makubwa katika mahusiano yake na mataifa mengine duniani baada ya kuwezesha mikakati ya utawala bora na uwekezaji kufaulu.

Na kwa upande fulani matunda yanaanza kuonekana mwaka huu kama mwendelezo wa miaka miwili iliyotangulia akiweka msingi wa ushirikiano kwa miaka inayokuja, hasa uchaguzi unapokaribia.

Kila safari aliyofanya Rais Samia haijakosa mafanikio na jitihada zake za utawala bora kwa kufungua ushiriki wa vyama vingi kwenye siasa hata kama ni kwa uangalifu, unawavutia wengi nje na ndani .

Kuelekea mwisho wa mwaka 2023 umekuja ugeni wa Rais Frank Walter Steinmeyer wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, ni ugeni muhimu kwani Ujerumani ndiyo hasa ilianza kuiunda Tanganyika na ilihusika katika matukio makuu ya wakati ule wa kuigawa na kuitawala Afrika.

Ujerumani iliweka mipaka ya nchi, ikaunda upya Utanganyika uliowaleta pamoja makabila na ukoo wa kila aina na kuleta hisia za utaifa na amani kwa watu wote ambao leo wanajivunia kuwepo kwa Tanzania licha ya historia kuwahusisha na kufanya ukatili mkubwa mfano kuharibu mifugo,kuvamia mashamba na kuyaharibu na kuua raia.

Ujio wa Rais wa Ujerumani na hitaji la kuomba radhi, mkuu huyo wa taifa lililoanzisha Tanganyika na leo Tanzania huenda lilishangaza.

Ukiangalia kinachowavutia wageni kuhusu Tanzania siyo kutembelewa na Rais Samia ila hata kufanya mikutano kadhaa ya kikanda na kimataifa katika jiji la Dar es Salaam kwa kufuatana ni kwa kuamini kuwa mwelekeo wake unaleta matumaini.



Rais Samia Suluhu Hassan na Kamala Harris, Makamu wa Rais wa Marekani. PICHA: IKULU

Suala hapa si kuleta matumaini kwa Tanzania peke yake ila zaidi kwa Afrika, kwani kila wakati nchi moja au nyingine inapanua au kufikisha demokrasia, ni Afrika ambayo inaangaliwa kwa mwelekeo huo, kwa mfano mapinduzi ya kijeshi nchi kadhaa za Afrika Magharibi, au kuondolewa kwa demokrasia shirikishi na awamu ya tano.

Wakati Tanzania inajua kasi ya maendeleo ya awamu ya tano huko nje walisikia kuwa demokrasia imekwama, umeingia mwelekeo wa kiimla, utawala mkali.

Unaweza kusema kuwa Rais Samia amefaulu kwa haraka kuridhisha matamanio ya nchi za nje ambazo zinashikilia kinachosemwa na upinzani kwa karibu, ila haielekei kuwa matazamio yake kuhusu kuinua uchumi wa nchi na kuleta maisha bora ni mkakati unaoweza kupata mafanikio kama huu wa kufungua nchi kidemokrasia.

Kuna tofauti kati ya mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi, ambako ukisikiliza lugha ya uongozi serikalini unagundua kuwa kuna aina ya utegemezi, bila kusema uvivu, wa kudhania kuwa kila kitu wananchi wanachohitaji kinaweza kupatikana.

Ukiangalia safari za nje na ujio wa wageni kutoka nje mwaka 2023, hakuna shaka ujio wa Makamu wa Rais Kamala Harris, wa Marekani, ulikuwa maalum.

Viongozi hao wawili ni wanawake wa kwanza kushika nafasi za juu za uongozi katika nchi hizi. Walifika hapo kwa njia zinazofanana, kwa kupewa nafasi ya mgombea mwenza, na katika nchi mojawapo kifo kikamwondoa rais aliyechaguliwa, hivyo makamu wake akachukua nafasi hiyo.

Ni jambo ambalo Rais Samia amekuwa akikumbushia hasa katika miaka ya awali ya utawala wake, kuwa Tanzania bado haijachagua rais mwanamke, ila ina nafasi ya kufanya hivyo uchaguzi ujao.

Akizungumza katika mkutano wa pamoja na waandishi wa habari, Rais Samia anaonyesha kufurahishwa na hatua ya Makamu wa Rais Harris kuipatia Tanzania kipaumbele alipoamua kufanya ziara fupi Afrika.

Kimsingi ni kuwa safari zinaandaliwa kuendana na uwepo wa maeneo mapana ya mafungamano, hivyo kwa upande huo kuna suala la kuwepo rais mwanamama, lakini pia dhamira ya kupanua ushiriki siasa kidemokrasia na kufungua milango ya uchumi katika maeneo tofauti.

Ukiangalia kwa karibu unakuta kuwa masuala ya uchumi hayajadiliwi kwa kina na viongozi wa Marekani ila kwa mikutano maalum, kwa mfano suala la kurefusha mpango wa biashara na Marekani bila ushuru wa forodha (AGOA) ambao unaelekea kumalizika 2025.

Pamoja na hayo iko mipango maalum ya Marekani kupunguza hatari ya magonjwa yanayoambukiza duniani ambako ulianzishwa Mpango wa Rais wa UKIMWI, TB na malaria, ambao sasa unaingia hatua nyingine ya magonjwa makuu ya ngono, ikiwemo homa ya ini (hepatitis).

Ujio wa Makamu wa Rais Harris uliwezesha pia kuongezewa mfuko maalum wa shughuli za haki za binadamu zinazoendana na uchaguzi bora kama msingi wa utawala bora.

Unaweza kusema kuwa mifuko hiyo imeanza kubadili hisia za upinzani, kuondoa masharti ya ushiriki siasa au demokrasia, ikiwa na maana kuwa utegemezi wa wadau kadhaa sasa umepungua, na sera za kutaka yote, kusema watakalo kuwa ndiyo demokrasia, inaisha.

Yako maeneo ya mahusiano hayo, ambayo hayakuanza na Rais Samia ila amefaulu kuyapa nguvu mpya, kwa mfano mkutano wa nchi za Afrika kutaka kongezwa muda AGOA zaidi ya mwaka 2025 uliongozwa na Tanzania na kufanyika jijini Dar es Salaam.

Isitoshe balozi wa sasa wa Marekani nchini, Michael Battle, wakati wa maandalizi ya mkutano wa AGOA alikutana na viongozi wa wafanyabiashara na sekta binafsi kuangalia uwezekano huo, na mazingira ya kukuza biashara na sekta binafsi kuwa na nafasi muhimu zaidi. Ilikuwa ni mara ya kwanza Balozi wa Marekani kukutana na wafanyabiashara tangu aondoke nchini baada ya kukaa miaka miwili balozi Robert Royall, mwaka 2004.

# Ukurasa katiba mpya unapofunguka 2024, iwe yenye muafaka, maridhiano ya kitaifa

**Na Gaudensia Mngumi**

KATIBA mpya ni jambo lililosikika na kutikisa sana mwaka 2023. Hata sasa Watanzania wanatamani na wana kiu ya kuona kikifanyika kitu, na jambo lao ni kuwa na katiba mpya.


Katiba kwa ujumla ni sheria kuu inayoongoza taifa. Iko juu ya mamlaka zote. Kila kitu kuanzia haki za raia, wajibu wa wananchi, taasisi kuu za dola, vyama vya siasa, mifumo ya kiuchumi na itikadi, uchaguzi na uteuzi wa viongozi wa ngazi zote na majukumu yao huanzia kwenye katiba.

Ndiyo inayowapa watalawa na wananchi uhalali wa kuongoza taifa, baada ya umma kukubaliana na mambo yote ya msingi yanayohitajika kudumishwa na kulindwa kikatiba.

Rais Samia Suluhu Hassan, tangu aingie madarakani, amefanya juhudi nyingi kuleta Tanzania mpya.

Akiongozwa na falsafa ya mambo manne au R 4- maridhiano, ustahimilivu, upatanishi, mageuzi na kujenga taifa endelevu linalohusisha ujenzi mpya wa pamoja.

Akisimamia falsafa hiyo Rais ameonyesha utayari wa taifa kuwa na sheria na pengine katiba mpya, akianza na kuunda kikosi kazi cha kuratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi.



Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea ripoti ya kikosi kazi cha uratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa kutoka kwa Mwenyekiti wake, Profesa Rwekaza Mukandala, Oktoba mwaka jana. PICHA: MTANDAO

Oktoba 2022 Rais Samia akapokea Ripoti ya Kikosi Kazi kuhusu Uratibu maoni ya wadau wa Demokrasia ya Vyama vingi vya Siasa, iliyokuwa inaongozwa na Mwenyekiti Profesa Rwekaza Mukandala.

Mwaka 2023 ukaanza kwa kuyafanyia kazi mapendekezo ya kikosi kazi kwa kuvifungulia na kuvitoa kifungoni vyama vya siasa kuanzia Januari. Mwaka 2017 vilipigwa marufuku na serikali ya awamu ya tano kufanya shuguli zozote za kisiasa.

Aidha, 2023 inapomalizika miswaada ya sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, Sheria ya Tume ya Uchaguzi na Sheria ya Vyama vya Siasa, imewasilishwa bungeni kwa ajili ya marekebisho.

Hatua hiyo, inakuja baada ya wadau mbalimbali wakiwamo wanasiasa kupeleka maoni yao kwenye Kikosi Kazi kilichoratibu maoni ya wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa.

Hata hivyo, licha ya kufikishwa bungeni sheria hizo, kuna dukuduku na wengine wakiguna kwa madai kuwa walipenda Rais asiwateue watendaji na viongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Wenye mtizamo huo kuanzia vyama vya siasa wanataka mkurugenzi wa NEC apatikane kwa kuomba nafasi hiyo, apatikane kwa uwazi, vigezo vianishwe,sifa na apate kazi baada ya kutuma maombi, kuchujwa na kukidhi vigezo kwa usaili si kwa uteuzi.

Ni pongezi kwa juhudi nyingi zinazofanyika matamanio ni kuona katiba mpya na sheria bora za uchaguzi zinapatikana na kama Wizara ya Katiba na Sheria ilivyoeleza kuwa katika bajeti yake ya 2023/24 suala la katiba limo.

Watanzania wanapovuka mwaka hoja ya katiba mpya na sheria rafiki za uchaguzi zipo vichwani mwao ni jambo muhimu ni kwamba vinapoandaliwa ni lazima viwe na muafaka na maridhiano ya kitaifa.

Na pia viandaliwe kwa ridhaa ya wadau walio wengi wawe wavikubali ili hata kama kutakuwa na malalamiko au hoja za kukosoa bado wengi wasimamie na kutetea.

Watanzania wengi hawatasema, lakini kuna ukweli kuwa wanaafiki kuwa katiba pendekezwa iliyoandaliwa na Bunge Maalumu la Kmwaka 2014 haikupata ridhaa wala makubaliano ya kitaifa.

Rais Samia Suluhu Hassan, tangu aingie madarakani, amefanya juhudi nyingi kuleta Tanzania mpya.

Inavyoelekea hata sasa inapingwa na wengi kwa hiyo kusiwe na haraka au papara za kufikia sheria za uchaguzi na katiba mpya wakati huu wa kuelekea uchaguzi wa 2024 wa serikali za mitaa na mkuu wa 2025, ambazo hazina maridhiano na kukubalika.

Baadhi ya wadau wengi wana maoni yakutoridhika na sheria kuhusu uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani, muundo wa NEC na sheria ya vyama vya siasa.

Ni wazi kuwa kuna hatua nyingi za kupita ili kuandaa na kupitisha katiba mpya hata sheria zinazofanyiwa marekebisho zinahitaji pia kufanywa kwa maridhiano si kulazimisha kwa sababu kutasababisha Watanzania kuendelea kwa miongo mingine tena kudai vitu hivyo upya.

Itakuwa ni kudai Tume Huru ya Uchaguzi , sheria ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani kadhalika na vingene vingi ambavyo havikuwaridhisha katika mchakato wa sasa.

Kama falsafa ya Rais ya maridhiano inavyosisitiza, kukubaliana kwa mambo yanayohusu demokrasia ya vyama vya siasa ni muhimu ili kazi ziwe na tija.

Ni dhahiri upungufu kwenye moja ya juhudi na kazi zinazofanyika, utasababisha mambo yasidumu na kazi isiwe endelevu.

Itakumbukwa katiba pendekezwa haikukubalika na vyama vya siasa vinavyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA).

Lakini, si UKAWA pekee hata baadhi ya viongozi wa kidini hawaikubali, vyama vya kiraia havikuiridhia, wajumbe wa Tume ya Kuratibu Maoni ya Katiba Mpya, wasomi na hata wananchi mmoja mmoja waliikosoa.

Kwa msingi huo inakosa uhalali wa kitaifa, haina maridhiano, inaonekana imejaa misimamo na ushabiki wa wachache.

MWaka 2024, unavyoanza badala ya kukimbia huku na huko ni wakati wa kukaa pamoja wadau wote na kukubaliana cha kufanya.

Dhamira inayowaongoza ni kwa sasa Tanzania inaongozwa na R4 hivyo kila jambo lipitie chujio hilo na kuwa na taifa linalodumisha falsafa za maridhiano, ustahimilivu, upatanishi, mageuzi na ujenzi endelevu mpya wa pamoja wa Tanzania.

Ikumbukwe katiba ni sheria ambayo iko juu ya yeyote, haifungamani na chama, dola wala kiongozi.

Ni sheria kuu na lazima iandaliwe na kuandikwa kwa kuridhiana kwa vile ndicho kiongozi cha viongozi cha raia wa taifa lote.

Ni vyema Rais na washauri wake waone kuwa ipo haja ya kukutanisha wadau kuanzia tasnia ya habari, wanasiasa, viongozi wa dini, wasomi, wataalamu wa sheria, wachumi, sekta binafsi, asasi za kiraia, mahakama, polisi, wanasiasa wastaafu na hata wataalamu kutoka Afrika na duniani katika kuamua haya mambo.

Wakubaline ni kipi cha kufanya na wapi pa kuanzia ili kuwa na katiba na sheria zenye ridhaa na makubaliano ya kitaifa.



# Kwa heri 2023 ulijaa yaliyoshangaza, ukiondoka na Watanzania 80 Hanang'

**Na Sabato Kasika**

ZIMEBAKI siku nne kuuaga mwaka 2023 ambao sasa unaelekea ukingoni, ulikuwa ni wa kusisimua kutokana na kujaa matukio mengi kuanzia kwenye siasa, kijamii na kiuchumi Wabongo wakilalamikia maisha kuzidi kuwa magumu.

Yapo ya kufurahisha lakini la kusikitisha zaidi tunapouacha mwaka 2023, kubwa linalozungumzwa ni vifo vya watu zaidi ya 80, majeruhi na uharibifu wa mali uliotokea Hanang' mkoani Manyara.

Ni maporomoko ya udongo kutoka mlima Hanang' yaliyotokoea usiku wa kuamkia Jumapili ya Desemba 3 na kuua zaidi ya watu 80 waliofunikwa na matope na kuharibu mali kuanzia nyumba, kuua mifugo, bidhaa madukani, magari, mazao shambani na miundombinu.

Ni ajali iliyotokea wilayani Hanang' mkoani Manyara sehemu kubwa iliyoathiriwa ni Kata za Gendabi na Katesh yalipo makao makuu ya Wilaya ya Hanang'.

Lilikuwa tukio lililoshangaza baada ya tope hilo kusambaa na kuzingira maeneo mengi likiwa linaporomoka kwa kasi likibeba miti, mawe na vitu vingine viliyosombwa na maji yaliyochanganyikana na takataka za kila aina kutoka mlimani na zilizokuwa ardhini.

Tangu wakati huo hadi sasa serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za binafasi na za umma, wanaendelea kutoa msaada wa kibinadamu kwa waathirika wa mafuriko hayo ambayo yameacha majonzi.

> Wengine ni Rais wa Sierra Leone, Julius Maada Wonie Bio, Rais Filipe Nyusi wa Msumbiji na Rais wa Malawi Dk. Lazarus Chakwera.

Tukio hilo linaweza kuwa ni la kufunga mwaka 2023 kutokana kwamba hakuna lingine la aina hiyo ambalo limetokea hivi karibuni zaidi ya hilo lililopoteza uhai wa Watanzania ambao ni zaidi ya 80.

Wakati huu wa kuelekea mwaka 2024, kilichotokea Hanang' kiamshe juhudi zaidi za kutunza mazingira ya milima kwa kupanda miti kwenye miteremko ya milima na ikibidi kuacha kufanya shughuli za kibinadamu kama kilimo na ufugaji wanyama wengi kwenye maeneo hayo.

Ikumbukwe kuwa kukata miti, kujenga na kubadilisha hali ya asili ya milima kunaweza pia kuchangia maporomoko ya udongo kwenye maeneo mengi bila kusahau kuwa Tanzania inaundwa na safu za milima.

Pamoja na ajali hiyo, Mei 12, taifa lilipata msiba wa kuondokewa na mwanadiplomasia na mtumishi wa umma aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Bernerd Membe. Mwanadiplomasia huyo aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wakati wa awamu ya nne na pia alihama CCM na kuwa mgombea urais wa chama cha ACT Wazalendo. Mwaka 2022, alirudisha kadi ya ACT-Wazalendo na kurejea tena nyumbani kwenye chama tawala.

Mwaka 2023 umeandika historia kwa Tanzania, iliyopokea ugeni wa Makamu wa Rais wa Marekani Kamala Harris aliyefanya ziara ya siku tatu, akitokea Ghana.

Mwezi huo wa Juni ulilishuhudia sakata la kuhoji mkataba wa uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam, kuendeshwa na kampuni ya DP World ya Dubai. Ni jambo lililosababisha mjadala kuanzia bungeni, katika vyombo vya habari, mitandaoni na hata katika nyumba za ibada.

Sakata hilo pia lilipewa nafasi kubwa kwenye mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, katika maeneo mbalimbali, huku baadhi ya wanasheria nao wakijitosa kulitolea ufafanuzi kulingana na jinsi walivyolielewa.

Sakata hilo lilimalizika Oktoba, baada ya Tanzania kutia saini mkataba na kampuni hiyo inayomilikiwa na Serikali ya Dubai ya DP World, ya kuendesha shughuli kwenye bandari ya Dar es Salaam....

Aidha, Agosti 22, Rais Samia Suluhu Hassan, alikuwa miongoni mwa viongozi waliohudhuria mkutano wa mataifa yanayoinukia kiuchumi duniani -BRICS yanayoundwa na Brazil, Urusi, India, China na Afrika Kusin, uliofanyika Johannesburg Afrika Kusini.

### NAIBU W/ MKUU

Agosti 30, Rais Samia anafanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri na kumteua Dk.Doto Biteko kuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati. Awali alikuwa Waziri wa Madini, aidha, anamteua January Makamba kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, akiondoka Wizara ya Nishati. Akamhamisha Balozi Pindi Chana kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Awali alikuwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo.

### SPIKA APAA

Oktoba 27, Spika Dk. Tulia Ackson, anachaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), katika uchaguzi uliofanyika jijini Luanda Angola.

Katika mkutano wa 147 wa umoja huo, Dk. Tulia anashinda uchaguzi mara baada ya kupata kura 172 ambazo ni sawa na asilimia 57 ya kura 303 zilizopigwa na wajumbe wanaoshiriki katika mkutano wa IPU, akiwashinda wagombea wengine watatu waliowania nafasi hiyo ambao ni Adji Diarra kutoka Bunge la Senegal aliyepata kura 59, Catherine Hara Spika wa Bunge la Malawi aliyepata kura 61 na Marwa Hagi kutoka Bunge la Somalia aliyepata kura 11.

Kwa ushindi huo, Dk. Tulia ni Rais wa 31 wa IPU na pia mwanamke wa kwanza kutoka Bara la Afrika kushika wadhifa huo, huku akiahidi kujitahidi kutimiza kile alichoaahidi wakati wa kampeni.

### KUNG'ARA KIMATAIFA

Mwaka huu ulikuwa ni wa marais wengi kuzuru Tanzania ambao walihudhuria mkutano wa wakuu wa nchi za Afrika kuhusu Rasilimali Watu (Africa Heads of State Human Capital Summit).

Mkutano huo ulifanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa Julai ukihudhuriwa na marais William Ruto wa Kenya, Rais Andry Rajoelina wa Madagascar na Rais Carlos Vila Nova wa São Tomé na Principe.

Wengine ni Rais wa Sierra Leone, Julius Maada Wonie Bio, Rais Filipe Nyusi wa Msumbiji na Rais wa Malawi Dk. Lazarus Chakwera.

Lakini pia walikuwamo Makamu wa Rais na Mawaziri Wakuu, katika mlolongo huo wa marais, Oktoba 30 Rais wa Ujerumani Frenk-Walter Steinmeier aliwasili nchini Oktoba 30 mwaka huu kwa ziara ya siku tatu ambayo ilimfikisha hadi Songea mkoani Ruvuma.

Lakini pia Novemba 16 Rais wa Romania, Klaus Lohannis, aliwasili nchini kwa ziara ya kitaifa kufuatia mwaliko wa Rais wa Samia ili kushawishi uwekezaji na kuvutia watalii wengi kutoka nchini Romania.

FATMA MNGWALI

# Diwani asiyeona anayeteswa na uduni wa miundombinu

## •Katika uzao wake anao watoto wanne wasioona

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

FATMA Mngwali Khamis (43) ni diwani mwanamama anayeishi na ulemavu, bila kujali hali yake amethubutu kugombea na kushinda udiwani wa viti maalum akitokea wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja.

Fatma haoni, lakini ni miongoni mwa madiwani 19 wanaounda Baraza la Manispaa Wilaya ya Kaskazini 'A', tisa kati yao ni wanawake.

Mkazi huyu wa Kijiji cha Fukuchani ni mama wa watoto saba, ambao wanne kati yao pia hawaoni kama yeye, tatizo analosema wanalipata wakifikia miaka miwili. Naye pia alipata upovu alipotimiza miaka hiyo.

Ni diwani pekee asiyeona miongoni mwa madiwani 165 walioko Unguja na Pemba.

Ripoti ya uchaguzi mkuu wa 2020 inayotolewa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), madiwani wanawake ni 77 sawa na asilimia 47,wa kuchaguliwa ni 22 na 55 ni wa viti maalum pamoja na wa kuteuliwa.

**KUFIKIA UDIWANI**

Safari yake ya kuusaka udiwani haikuwa rahisi hata kidogo alikumbana na changamoto nyingi zilizoelekea kukatisha ndoto zake.

Hata hivyo, bila kujali ulemavu wake, alipambana akawa mwanamke wa kwanza asiyeona kushika nafasi hiyo katika historia ya siasa za vyama vingi Zanzibar.

"Haikuwa rahisi kufika hapa nilipo, niliandamwa kwa maneno ya kejeli na dharau wakati wa kampeni katika kwa sababu ya hali yangu," anasema.

"Waliniambia kama sioni vipi naweza kuwa kiongozi? Niliumia kwa sababu sikuomba kuwa mlemavu. Niliamua kuwapuuza nikiamini katika uwezo wangu licha ya ulemavu nilionao."

Anasema, licha ya vikwazo alivyopitia, alichaguliwa kuwa diwani wa viti maalum na kwa mara ya kwanza Disemba 12, 2020 alikula kiapo.

**MAJUKUMU**

Nipashe inataka kujua suali la kwanza analouliza katika kikao cha Baraza la Manispaa. Akijibu, anasema aliuliza jinsi gani watu wenye ulemavu wanajumuishwa katika mipango ya manispaa?

Anafahamisha kuwa, anafanya kazi kubwa ya kutetea wanaoishi na ulemavu ili kuhakikisha haki na fursa sawa zinapatikana na kwamba hakuna kati yao anayeachwa kwa sababu za kimaumbile.



Fatma Mgwali Khamis Diwani wa viti maalum Wilaya ya Kakazini A Unguja. PICHA: RAHMA SULEIMAN

Anataja msaada anawapa kuwa ni kufanya makongamano na mikutano kila mwaka kuzungumzia changamoto za wenye ulemavu na baadhi zimepatiwa ufumbuzi na serikali.

Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana kutokana na makongamano yake, ni ujenzi wa shule zenye mahitaji ya watu wenye ulemavu Unguja na Pemba.

"Pia kumeundwa mabaraza ya wenye ulemavu katika kila wilaya ili kutatua changamoto zinazowakabili," anasema.

**CHANGAMOTO BARAZANI**

Fatma anaiambia Nipashe kuwa katika vikao vya baraza hilo vikiwemo vya kupitisha bajeti, karatasi zinazotumika zinakuwa na maandishi ya kawaida. Hali hii inamkwamisha kuwa na uwezo wa moja moja wa kuchangia mijadala.

Maandishi pekee ambayo yangemsaidia ni ya nukta nundu (braille), ambayo hata hivyo mashine za kuchapia maandishi hayo hazipatikani katika vikao vya baraza.

"Kwangu nisiyeona hili ni tatizo kubwa na nisipokuwa na msaidizi wa kunisomea siwezi kuelewa kilichoandikwa na hivyo uwezo wangu wa kushiriki mijadala muhimu kama kupanga bajeti za maendeleo ya manispaa unakuwa mdogo," anabainisha.

Anataja sababu nyingine zinazofanya ashindwe kushiriki kikamilifu katika mijadala ni kukosa kifaa cha kurikodia sauti (voice recorder).

Mahitaji ya watu wenye ulemavu katika manispaa anayofanyia kazi, hayajazingatiwa kwani hata vifaa hivyo visaidizi kwa wasioona hakuna.

"Nikiwa barazani siachi kupiga kelele kutaka viongozi waone umuhimu wa kutafuta vifaa hivyo lakini inaonesha viongozi wetu hawana uelewa hivyo hawalipi kipaumbele jambohilo," Fatma anaeleza kwa masikitiko.

Anashauri kuwepo mafunzo kwa watendaji wa serikali wakiwamo meya na wakurugenzi katika mabaraza ya manispaa ili waelewe uhalisia wa magumu ambayo wenye ulemavu wanakutana nayo.

Anasema mafunzo hayo yatawapa uelewa na hivyo kutenga nafasi za uajiri kwa ajili ya watu kutoka kundi hilo pamoja na kusaidia upatikanaji wa mahitaji yao.

**NENO WENYE ULEMAVU**

Ili kupata ushiriki mpana wa wanawake wenye ulemavu katika uongozi hasa wa kisiasa, Fatma anawashauri wajiunge na makundi ya kisiasa na kushiriki harakati ngazi za chini ili kujijengea mazingira mazuri ya kukubalika pale wanapoamua kugombea uongozi

"Kujiegemeza katika makundi ya kisiasa na jumuiya zake, tunarahisisha kujisafishia njia ya kushinda kuliko kuibuka moja kwa moja na kutaka kugombea udiwani, uwakilishi na ubunge," anatoa rai.

**FIKRA POTOFU**

Anasema mara kadhaa kumekuwa na mtazamo unaosemwa sana kwamba adui wa mwanamke katika kufikia maendeleo ni mwanamke mwenzake.

Lakini, Fatma anapinga mtazamo huo anaodai unalenga kuwarudisha nyuma wanawake. Haachi kuwashukuru wanawake wenzake kwa kumuunga mkono na kusimama naye hadi kuukwaa udiwani.

"Kutokana na harakati zangu wanawake wenzangu ndiyo walionishawishi na kunipa moyo wa kugombea nafasi hii kuliko wanaume," anaweka wazi.

Anasema kwa sasa anatamani kuona siku moja nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali Bara na Zanzibar zinashikwa kwa uwiano sawa wa 50/50 kati ya wanawake na wanaume.

**UONGOZI WASIOONA**

Upi mtazamo wa Jumuiya ya Wasioona Zanzibar (ZANAB) juu ya wanawake wenye ulemavu katika uongozi?

Adil Mohammed Ali ni Mratibu wa ZANAB Zanzibar, anasema wanawake wengi wenye ulemavu hawapati nafasi za uongozi kutokana na maumbile na hali zao, kwa kuonekana wana uwezo mdogo.

Anasema hata katika vyombo vya maamuzi mfano Baraza la Wawakilishi na lile la madiwani, wanawake wenye ulemavu wametengewa nafasi chache.

"Hii inaonesha kuwa bado watu wenye ulemavu hawajapewa kipaumbele kwa vile jamii inawaona hawawezi," anaeleza.

Hivyo, anavishauri vyama vya siasa kuwaendeleza wanawake hasa wenye ulemavu na kutengeneza miundombinu ya kuwafikisha kileleni.

Aidha ,anavihimiza vyombo vya sheria kuandaa mazingira mazuri kwa watu wenye ulemavu ili wanapoingia katika nafasi za uongozi kusiwe na vikwazo wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Wanawake wenye ulemavu wana uwezo, wanapopata nafasi za uongozi huzitendea haki wakizitumikia kwa bidii na weledi, Ali anaongeza.

"Hata diwani Fatma Mngwali mwanachama wetu ZANAB, anafanya kazi kubwa, anaitendea haki nafasi yake na jumuiya yetu yenye wanachama 536, wanawake wakiwa 256 na wanaume 280, ambao wote hawaoni."Anasema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, Salma Haji Saadat, anasema jumuiya inawasadia ili wafaidike na kushiriki mijadala na mambo mbalimbali ya kijamii.

Anasema jumuiya huwashawishi na kuwaunga mkono kugombea nafasi za uongozi na kuwajengea uwezo na ujasiri wa kujiamini.

Anasema kwa sasa jumuiya inaendesha programu ya kuwapa mafunzo wanawake wenye ulemavu watiania kugombea nafasi za uongozi ili uchaguzi wa 2025 kuwe na idadi kubwa kutoka kundi hilo katika vyombo vya maamuzi. Anawashauri wanawake wenye ulemavu kuanzia uongozi ngazi za chini badala ya kuwaza kupaa juu moja kwa moja, akisema ni vigumu iwapo hakuna maandalizi ya kutosha.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar Ussi Khamis Debe, anasema pamoja na jitihada za kusimamia haki na fursa za kundi hilo, bado mwitikio wa jamii kuwapaisha ni mdogo hasa kwenye kugombea uongozi.

Anaeleza kuwa jitihada mbalimbali zinafanywa kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo, ikiwamo kuweka misingi imara ya kuhakikisha wananufaika na fursa zote zikiwemo za uongozi.

Anavishauri vyama vya siasa kuweka mazingira wezeshi kwa wenye ulemavu na kujenga imani kwao ili wanapoingia kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi kusiwe na vikwazo.

Akimzungumzia diwani Fatma, Debe anampongeza kwa kujitoa na kupambana kupata nafasi hiyo na kutetea wasiiona.

Meya wa Baraza la Manispaa Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Machano Fadhil Babla, anasema licha ya mazingira yasiyo rafiki kwa madiwani wenye mahitaji maalum, washiriki kikamilifu shughuli za kiofisi na jamii.

Babla, anakiri kuwa hakuna vifaa visaidizi ikiwemo mashine za maandishi ya nukta nundu ili kumrahisishia Fatma na jamii ya wasioona katika manispaa hiyo kutekeleza kazi zao.



# Kundi maalum laombewa kukumbukwa sikukuu

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MWENYEKITI Jumuiya ya Maridhiano na Amani Tanzania (JMAT), Dk. Askofu Evance Chande, ameziomba Taasisi za dini, mashirika na watu binafsi wenye uwezo kuwakumbuka yatima, wajane, wenye ulemavu na wasiokuwa na uwezo wakati huu wa msimu wa sikuku za mwisho wa mwaka.

Alisema, jamii hizo wakati wa kipindi kama hiki zinasahaulika kwenye Sikukuu ya Krismasi na mwaka mpya kwa kutopatiwa mahitaji muhimu yakiwamo chakula na mavazi.

Dk. Chande, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza kwa ibada ya Sikukuu ya Krismasi iliyofanyika Kanisa la Karmel Assemblies of God, Ipagala jijini hapa.

Aliziomba taasisi, mashirika watu binafsi kwenye kipindi hiki watumie nafasi zao kuwajali na kuwakumbuka wenye mahitaji na kuwasaidia.

"Kwenye kipindi hiki ambacho sikukuu jamii hizo zimekuwa zikisaulika na familia zenye uwezo badala ya kuwakumbuka na kula nao chakula pamoja," alisema.

Awali, akihubiri katika ibada ya Krismasi aliwakumbusha wazazi na walezi kuwakumbuka watoto kwa kuwaandalia mahitaji ya elimu kwa wanaotarajiwa kuanza masomo shule zitakapofunguliwa.

Alisema wazazi na walezi ni muhimu wakakumbuka umuhimu wa kuwaandalia mapema vifaa vya shule ili kuondokana na changamoto za kuwakwamisha kutojiunga kwa wakati kwenye masomo.

Aliwataka waumini wa kanisa hilo kuendelea kufanya maombi kila siku ili kuwezesha kazi ya kiroho ya kuwahudumia watu ipate majibu kutoka kwa Mungu.

# Wanafunzi wanaofanya vizuri kusaidiwa na mkoa

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKOA wa Singida unatarajia kuanzisha Mfuko wa Elimu utakaokuwa maalum kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wanaofanya vizuri kimasomo na wanaoshindwa kuendelea na shule kutokana na wazazi wao kutokuwa na uwezo wa kuwasomesha.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alitangaza mpango huo hivi karibuni kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) baada ya kubainika kuwa baadhi ya wanafunzi wanaofaulu wanashindwa kuendelea na masomo ya sekondari kutokana na wazazi wao kutokuwa na uwezo.

"Tukitaka watoto wetu wafanya vizuri na ufaulu uongezeke ni lazima tuanzishe mfuko wa elimu wa mkoa ambao utakuwa ukiwasaidia wanafunzi ambao wanafanya vizuri kwenye masomo lakini wazazi wao hawana uwezo wa kuwasomesha," alisema.

Serukamba alisema utaratibu wa kuwabaini wanafunzi hao ambao wazazi wao hawana uwezo utafanyika kuanzia kwenye maeneo wanayoishi kupitia kwa viongozi wa kitongoji, kijiji na kata na walimu wakuu wa shule.

Alisema mambo yatakayoweza kuongeza ufaulu wa watoto ni kufanyika kwa vikao vya mara kwa mara na Wakuu wa wilaya, Maofisa Elimu Kata, Madiwani na Watendaji kata kutokana na utoro wa wanafunzi kuanzia shuleni hadi nyumbani na kuongeza upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi wakiwa shuleni.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema mpango huo ni mzuri na unawezekana kwa asilimia 100 na kutoa mfano kwa Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma ambayo ilifanikiwa katika jambo hilo.

"Jambo kama hili linafanyika pale Bahi na fedha zinapatikana kupitia vibali vya mifugo ambayo ilikuwa inaleta mapato karibu asilimia 60 katika minada kwa kila ng'ombe anatozwa Sh. 2,000 na baadaye suala hilo lilipitishwa kwenye Baraza la Madiwani na kiwango kikaongezwa kutoka Sh. 2,000 hadi 4,000," alisema.

Dk. Mganga alisema baada ya kupata fedha hizo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi alikuwa akipita kwenye vijiji na kata kuwa hawana shida ya kuwapeleka watoto shule kutokana na kuwapo kwa mfuko huo wanachohitajika ni mtoto afaulu ananunuliwa mahitaji yake yote ya shule na fedha za mfuko huo.

Alisema Singida wanaweza kuangalia moja ya chanzo cha mapato ambacho ni kizuri nao wakakifanya kama walivyofanya Wilaya ya Bahi na fedha zitakazokuwa zinakusanywa zitawasaidia watoto wa wilaya husika.



Ofisa Mtendaji wa Kata ya Endiamtu, Mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Charles Msangya (katikati) akielezea mikakati ya elimu kwa wazazi na walezi wa shule za msingi na sekondari kuchangia chakula juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Washauri matumizi salama viuatilifu kuongeza uzalishaji

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WANACHAMA wa Chama cha Taaluma ya Sayansi Kilimo na Mazao Tanzania (CROSAT), wameshauri kuwapo kwa mfumo bora wa mbegu, matumizi salama ya viuatilifu ili kuongeza uzalishaji katika sekta ya kilimo.

Walisema hayo juzi wakati wa mkutano mkuu wa pili wa mwaka wa matumizi sahihi ya mbegu na viuatilifu ni miongoni mwa ajenda zilizojadiliwa kwenye mkyano huo.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Prof. Maulid Mwatawala, alisema watafiti na wanachama wa CROSAT wakitumia taaluma zao kufanya utafiti na kutoa elimu sahihi ya viuatilifu wataisaidia sekta hiyo nchini.

"Mimi niko kwenye afya ya mimea, tunafanya tafiti zinazomsaidia mkulima hasa katika visumbufu vya mmea, wakulima wengi wanatumia viuatilifu visivyo sahihi au kutumia kwa kiwango kikubwa kuliko kinachotakiwa na matokeo yake kuathiri mazingira, afya ya mlaji na mazao yenyewe," alisema.

Alisema, kuna njia mbadala ikiwamo matumizi ya wadudu rafiki na njia mbadala ya kilimo.

Kadhalika, alisema watafiti wanafanya kazi kubwa kuhakikisha masoko ya kimataifa yanapatikana ambayo yanategemea kusafirisha bidhaa ambayo haijaathirika na wadudu.

"Hivi karibuni Tanzania ilipata soko la parachichi nchini India na nchi nyingine, hapo mwanzo tulifungiwa zaidi ya miaka 10, kutokana na kuwepo na visumbufu waliona tunaweza kupeleka visumbufu katika nchi zao," alisema.

"Parachichi ilikuwa ikisumbuliwa sana na nzi waharibifu wa matunda, lakini hivi karibuni Wizara ya Kilimo ilitoa mwongozo wa jinsi gani tunaweza kuendeleza tasnia ya parachichi na namna ya kudhibiti magonjwa na wadudu na magugu ili kuweza kulima parachichi kwa tija na kiwango kinachofaa," alisema.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), Prof. Joseph Ndunguru, alisema lengo la mkutano huo ni kubadilishana uzoefu na taaluma hasa kuongeza tija.

Alisema kama mwanachama na Mkurugenzi mkuu wa mamlaka moja ya kazi zao ni kusimamia matumizi ya viuatilifu na afya ya mimea.

Kadhalika, uwapo wa chama hicho ni muhimu kwa kutumia jukwaa wanachama wanapata taarifa kuhusu yanayofanyika kwenye sekta ya kilimo na kuleta mageuzi.

"Kwenye kilimo matumizi ya viuatilifu ni muhimu ili vitumike kwa usahihi na kuleta matokeo mazuri," alisema.

Mwenyekiti wa mkutano huo ambaye pia ni Mhadhiri Mwandamizi wa Idara ya Sayansi ya Mazao na Kilimo cha bustani katika Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA) Morogoro, Prof. Kallunde Sibuga alisisitiza umuhimu wa mfumo bora wa mbegu na matumizi salama ya viuatilifu.

Alisema kuwa CROSAT inalenga kushughulikia masuala muhimu yanayoathiri uzalishaji wa mazao na upatikanaji wa chakula cha uhakika kwa Tanzania.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa CROSAT, Patrick Ngwediagi, kuna haja ya kuwa na mfumo thabiti wa mbegu utakaowezesha upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima.

Pia, inaangazia umuhimu wa matumizi salama ya viuatilifu, kuhakikisha ulinzi wa afya ya binadamu na mazingira.

"Kwa kuwa katiba iliyorekebishwa ipo, CROSAT inathibitisha tena jukumu lake katika kutetea sera na mipango inayounga mkono malengo haya," alisema.





# Viongozi wa dini waviasa vyama vya siasa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa dini mkoani Mbeya wamevitaka vyama vya siasa nchini kuepuka misuguano na migogoro ndani ya vyama vyao wakati taifa linapoelekea kwenye uchaguzi wa viongozi wa serikali za mitaa mwakani ili kuepusha machafuko.

Vyama hivyo vemevitakiwa viweke mazingira mazuri yatakayowezesha Watanzania kupata viongozi bora kwa njia halali ya kidemokrasia bila kuathiri amani na utulivu kwenye jamii.

Akihubiri ibada ya Krismasi, Makamu Askofu wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) mkoani Mbeya, Mchungaji Dk. Hurdson Mwaijunga, alisema ili Watanzania wapate viongozi bora wanaowataka ni lazima kuwapo na utulivu mzuri ndani ya vyama vya hivyo.

"Tunatambua kuwa taifa letu linaelekea kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani, hivyo tunashauri vyama vya siasa visiwe na misuguano ndani ya vyama vyao na badala yake viweke mazingira mazuri ya kupata wagombea watakao wania nafasi za uongozi kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao utafanyika mwakani," alisema Dk. Mwaijunga.

Askofu Hurdson Mwaijunga ambaye pia ni Kiongozi Mkuu wa Kanisa la TAG, Jerusalem Temple la Sokomatola, jijini hapa, alisema kuna mambo mawili ambayo Watanzania hawapendi kuyaona wakati wa uchaguzi.

Aliyataja kuwa ni misuguano miongoni mwa wanasiasa hasa wanaotoka ndani ya chama kimoja kubaguana wakidhani kuna watu maalum wa kuwa viongozi na wengine hawafai.

Alisema kila binadamu amepewa karama yake na Mungu, kila anayehitaji kuonyesha kipaji chake cha uongozi na kufuata njia halali za kidemokrasia aachwe atimize ndoto zake.

Dk. Mwaijunga alilitaja jambo la pili kuwa ni rushwa kwenye uchaguzi aliodai kuwa Mtanzania hapendi utaratibu wa rushwa na mambo mengine yanayokinzana na sheria za nchi na utamaduni wa kitanzania.

Aliiomba serikali kuzuia mambo kama hayo kwa nguvu zote ili chaguzi zinaokuja zifanyike kwa haki, utulivu na amani.

Ibada hiyo pia ilihudhuriwa na viongozi wa dini kutoka nchi jirani ya Malawi, ikiwa ni sehemu ya kuimarisha ujirani mwema.

Askofu Daniel Masamba wa Kanisa la TAG la Lilongwe nchini Malawi, alisema uhusiano mzuri baina ya Tanzania na nchi yake unasaidia kuimarisha uchumi na huduma za kiroho baina ya wananchi wan chi hizo mbili.

Alisema uhusiano wa muda mrefu wa nchi hizo mbili umesababisha kuwapo na undugu baina ya wananchi wa pande zote mbili na kufikia hatua ya kushiriki pamoja mambo ya kiroho.

"Kuna Watanzania wengi wanakuja Malawi kufanya biashara na pia wapo Wamalawi wanaovuka mpaka kuingia Tanzania kufanya biashara, jambo hili ni zuri kwa kuwa limetufanya kuwa kama familia moja na kuanzisha hata ushirikiano wa kiroho kwenye makanisa yetu," alisema Askofu Masamba.

Juzi, watanzania waliungana na waamini wengine wa dini ya kikristo duniani kote kusherehekea Sikukuu ya Krismasi ya kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Bwana wao.



Ofisa elimu msingi, Doroth Mwandila (kulia) akieleza kwa wageni wake jinsi chumba cha darasa kilivyojengwa kwa ustadi na ubunifu wa hali ya juu.**PICHA: YASIN IBRAHIM**

## H'shauri Mbeya, CRDB kuanzisha mfumo kisasa ukusanyaji mapato

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MIEZI kadhaa baada ya kuibuka kwa mfumo feki wa ukusanyaji wa mapato kwenye baadhi ya halmashauri nchini na kusababisha upotevu wa fedha za umma, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya imeingia makubaliano na Benki ya CRDB kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa kisasa wa ukusanyaji wa mapato hayo.

Mfumo huo unatarajiwa kutumika kwenye baadhi ya maeneo ikiwamo stendi ya mabasi ya Mbalizi na watu wote wanaotakiwa kulipa mapato watakuwa wanapatiwa namba ya malipo na kulipa kupitia mfumo huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Stephen Katemba, alisema mfumo huo utafungwa kwenye mageti yanayotumika kukusanya ushuru wa mazao.

Alisema mfumo huo ukianza kutumika hakutakuwa na upotevu wa mapato kwa maelezo kuwa wakusanyaji wa mapato hayo hawatakuwa wanapokea fedha kwa walipa ushuru na badala yake zitakuwa zinalipwa moja kwa moja kwenye mfumo.

"Kwa sasa tunauweka kwenye baadhi ya maeneo na tutakapoona una mafanikio tutauweka na kwenye maeneo mengine yote ambayo tunakusanya mapato," alisema Katemba.

Alisisitiza kuwa mfumo huo utasaidia pia kupunguza migogoro kati ya halmashauri na mawakala ambao unatumika kukusanya mapato. Meneja Biashara wa Benki ya CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Japhar Asanary, alisema mfumo huo umebuniwa na wataalamu wa benki hiyo.

Alisema watahakikisha mawakala wa benki hiyo wanawekwa kwenye maeneo yote ya ukusanyaji wa mapato ili kurahisisha utendaji kazi wa mfumo huo.

Aliipongeza halmashauri hiyo kwa kuendelea kutumia huduma za benki hiyo na kwamba watahakikisha wanafanya kazi kwa karibu na halmashauri ili kuhakikisha mfumo unaleta mafanikio.

# DC ataka jamii kuungana kampeni tokomeza udumavu

**Na Elizabeth John,** MAKETE

MKUU wa Wilaya ya Makete, Mkoa wa Njombe, Juma Sweda ametoa rai kwa jamii wilayani humo kuungana katika kampeni ya kupambana kutokomeza udumavu.

Rai hiyo aliitoa wakati wa Mkutano Mkuu wa Chama cha Maendeleo Makete (MDA), uliofanyika wilayani hapa.

Sweda alisema, Mkoa wa Njombe unakabiliwa na changamoto ya udumavu na kwamba kuna haja ya hatua kuchukuliwa.

"Suala la lishe bora ni changamoto inabidi watu wajue sababu ya udumavu ni kuanzia mtoto miaka sifuri ndiyo tatizo linakuwa kubwa sana, unakuta mtu haelewi analalamika kumbe ni udumavu," alisema Sweda.

Alisema jamii isipopambana na udumavu kuanzia umri wa mwaka 0 hadi mitano kutakuwa na kizazi kilichodumaa moja kwa moja na mwanamke atakuwa na nafasi kubwa ya kutozaa mtoto aliyedumaa.

Alisema wakati umefika kwa watu wa Makete waliopo nje kurudi na kufanya mageuzi katika uwekezaji kwenye sekta za kilimo, majengo na utalii katika hifadhi ya Kitulo.

Awali, Mwenyekiti wa Chama Cha Maendeleo Makete (MDA), Clement Sanga alisema chama hicho kipo tayari kuunga mkono jitihada za wilaya za kutokomeza udumavu kwa kutoa ng'ombe wa maziwa shuleni.

"Hiki ni chama cha hiari, lakini ni kwa ajili ya kujiletea maendeleo katika wilaya yetu hasa jamii ya wanamakete ambao wako nje, lakini ambao wako hapa," alisema Sanga.

Katibu wa Chama cha Maendeleo cha Makete (MDA), Award Mpandila, alisema ili kufanya Makete kuwa ya mabadiliko, tayari wanahamasisha kujenga nyumba bora pamoja na kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe, alisema wamekusudia kuifanya wilaya hiyo kuwa kitovu cha uzalishaji wa zao la ngano nchini.

"Tani 1,000 zitalimwa kwenye hekta 14,000 na kwenda kuokoa bilioni 551 zinazotumika kuagiza malighafi nje ya nchi, pia tunaishukuru kwa hatua ya kupimiwa udongo katika mashamba yetu ili kuanza kilimo, alisema Mkufwe.



# Wajasiriamali wanawake waonyeshwa fursa maendeleo

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Siti Abasi Ali, amewataka wajasiriamali wanawake kuzitumia fursa mbalimbali za maendeleo zinazotolewa na viongozi wao.

Aliyasema hayo jana Dunga katika kikao cha kuwahamasisha kujiunga na majukwaa ya wanawake, yanayotarajiwa kuanzishwa katika wilaya na shehia.

Aliwataka kutumia fursa iliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kuanzisha majukwaa hayo ambayo yatasaidia kuwaletea maendeleo.

Aidha, alisema lengo la Rais Samia kuanzisha majukwaa hayo, kila mwanamke anafikiwa kimaendeleo na kuepukana na tatizo la umaskini.

Alisema majukwaa hayo yatasaidia pia kuwaweka pamoja wajasiriamali wa fani mbalimbali na kuanzisha miradi itakayoweza kuwasaidia.

Aliwataka wenyeviti, makatibu na washika fedha wa vikundi hivyo, kuwahamasisha wanawake wenzao wajiunge katika vikundi ili kupata fursa zinazotolewa.

Ofisa jinsia kutoka Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ashura Suleiman Juma, aliwataka wajasiriamali hao kuanzisha miradi inayotoa fursa ya kuzalisha bidhaa zenye ubora ili kupata soko la uhakika. Aliwataka viongozi wa vikundi hivyo kufanya tathmini ya vikundi vyao ili kujua idadi yao na mahitaji katika vikundi hivyo.

Wajasiriamali wanawake katika wilaya hiyo waliahidi kujiunga na majukwaa hayo ili kupata miradi itakayowaletea maendeleo na kuhamasisha wanawake wenzao kujiunga na jukwaa hilo ili malengo yaliyowekwa na serikali yaweze kufikiwa.

# SMZ kuhamasisha matumizi gesi, umeme

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maji, Nishati na Madini, Shaibu Hassan Kaduwara, amesema Serikali ya Zanzibar itaendelea kuhamasisha wananchi kutumia nishati ya gesi na umeme ili kupunguza athari za uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji wa misitu.

Aliyasema hayo jana wakati akikabidhi mitungi ya gesi ya kupikia kwa wananchi wa vijiji vitano vya Unguja, Mkoa wa Kusini.

Mitungi hiyo imetolewa na Shirika la kuwawezesha wanawake kiuchumi na kielimu (FAWE) kwa kushirikiana na kampuni ya ORYX Gas pamoja na mamlaka ya udhibiti wa maji na nishati Zanzibar (ZURA).

Vijiji vilivyopatiwa mgao wa mitungi ya gesi ni Uroa, Uzi Ngambwa pamoja na Makunduchi, Jambiani Mkoa wa Kusini, Unguja.

Waziri Kaduwara alisema Zanzibar inaungana na nchi nyingine za bara la Afrika zenye mikakati ya kupunguza matumizi ya kuni kwa ajili ya kupikia.

Alisema matumizi ya kuni yamesababisha athari kubwa kutokana na baadhi ya maeneo kukumbwa na ukame na kukosa mvua kutokana na ukataji wa msitu wa kupindukia.

Alisema serikali inaendelea kukamilisha mikakati yake ifikapo mwaka 2030 wananchi wa Zanzibar wawe tayari wanatumia umeme na gesi kwa ajili ya shughuli zao nyingi ikiwamo za kupikia.

"Mikakati yetu ifikapo mwaka 2030 kuona kwamba tunatumia nishati ya umeme pamoja na gesi kwa matumizi yetu ya kawaida ikiwamo majumbani na kuachana na kuni na mkaa ambazo athari zake kwa mazingira ni kubwa," alisema.

Mjumbe wa bodi ya FAWE, Sabrina Omar Abdalla, alisema taasisi hiyo imeona upo umuhimu wa kutoa mitungi hiyo kwa ajili ya kuwawezesha wanawake kiuchumi na kuacha matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema matumizi ya kuni na mkaa athari zake katika mazingira ni kubwa, wakati umefika kuwapo kwa matumizi ya gesi na umeme kutunza mazingira ya baadaye kwa faida ya vizazi vya sasa na vijavyo. "Tumejipanga kuona wanawake wanatumia nishati ya umeme na gesi kwa ajili ya kulinda mazingira yetu ya baadaye na vizazi vyetu," alisema. Meneja Mkuu wa kampuni ya ORYX Tanzania, Benoit Araman, alisema wanahitaji kuona matumizi salama ya nishati ya gesi kwa maendeleo ya Tanzania na wananchi wake.

Alisema taasisi yake itaendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kulinda mazingira na kulinda hifadhi ya msitu kwa ajili ya kutunza vyanzo vya maji safi na salama.

"Tunatakiwa kupunguza kwa kiasi kikubwa ukataji wa miti kwa matumizi ya nishati ili kulinda mazingira na athari za kutoweka kwa vyanzo vya maji safi na salama," alisema.

Halima Bakari, mkazi wa kijiji cha Uroa, Wilaya ya Kati Unguja ni miongoni mwa wanufaika wa majiko hayo, alisema amefurahishwa kupata mtungi wa gesi ambao atautumia kwa shughuli za nyumbani na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Majiko 60 yametolewa na wadau ikiwa ni utekelezaji wa mradi wa kuwawezesha wanawake kiuchumi unaotekelezwa na UN Women katika kuunga mkono mikakati ya serikali ya kupunguza athari za mazingira za ukataji wa kuni na matumizi ya mkaa.



Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga-Bombo, Dk Naima Yusuf (kushoto) akigawa zawadi za Sikuu ya Krismasi na Mwaka Mpya kwa Ofisa Takwimu wa Hospitali hiyo, Rashid Lukumbuja juzi ikiwa ni utamaduni wao waliojiwekea kila sikuuu kubwa kufanya hivyo. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Jamii yatahadharishwa kuiga utamaduni wa kigeni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, ameitaka jamii kuacha tabia ya kuiga tamaduni za kigeni ambazo haziendani na mila,silka na utamaduni wa kizanzibari ikiwemo suala la mavazi na malezi.

Waziri Pembe aliyasema hayo katika maonesho ya mavazi ya wiki ya Mafunzo ya Amali yaliyofanyika katika viwanja vya Mapinduzi Square, Michenzani Mjini Unguja.

Alisema mavazi ya staha na heshima ni moja ya utamaduni wa Wazanzibari na kwamba ni vyema kuendelezwa na kuacha kuiga mavazi ambayo hayanastaha.

Aidha, alisema mavazi ya staha na malezi bora ni njia moja wapo ya kuzuia vitendo vya ukatili na udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto ambavyo vinajitokeza kila mara ndani ya jamii.

"Suala la kuiga tamaduni zisizo za kizanzibari ambazo baadhi yake ndio sababu kubwa ya mporomoko wa maadili ya nchi na kusababisha vitendo vya udhalilishaji kuongezeka kila siku ni vyema kuachana nazo na badala yake kuendeleza mila, silka na utamaduni wa Zanzibar," alisema.

Pembe aliitaka mamlaka ya mafunzo ya amali pamoja na vyuo vingine vya ufundi kuanzisha madawati ya kijinsia katika vyuo vyao ili iwe rahisi kwa wanafunzi wanapopata tatizo au kuona viashiria vya udhalilishaji kutoa taarifa kwa haraka kuhusu kupinga vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Aliwataka wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao katika vyuo hivyo ili kupata taaluma na ujuzi utakaowasaidia vijana kupata ajira na kujiongezea kipata hali ambayo itawasaidia kuinuka kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Bakari Ali Silima, alisema maonesho ya mavazi ni kazi zinazofanywa na vyuo hivyo, ni vyema jamii kuangalia ili kujifunza na kuona ni sehemu sahihi ya kuwapeleka watoto wao kupata ujuzi.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa mavazi hayo, Fatma Ali alisema vazi la staha linasaidia kumpa mtu ujasiri wa kukutana na watu mbalimbali katika harakati za maisha na mavazi ni mawasiliano katika jamii husika.

# Wote wanaoabudu mizimu watakiwa kumrudia Mungu

**Na Steven William,** MUHEZA

PADRI wa Kanisa Katoliki la Kristo Mfufuka wilayani Muheza, Martine Kihiyo, amewataka wakristo kuacha tabia ya kujihusisha na shughuli za uganga wa kienyeji na kuabudu mizimu wanapopatwa na matatizo na badala yake wamrudie Mungu.

Aliyasema hayo juzi katika ibada ya Sikukuu ya Krismasi baada ya kusema kuwa wapo wakristo wanaopokea sakramenti kanisani, lakini wanapokuwa nje ya kanisa wanajishughulisha na uganga wa kienyeji na kuabudu mizimu chini ya miti na kumsahau Mungu.

Aliwataka kujenga mazoea ya kupeleka matatizo na shida zao kwa Mungu badala ya kuabudu mizimu chini ya miti.

Kadhalika alisema mkristo yeyote anayekula sakramenti halafu anajihusisha na shughuli za uganga wa kienyeji na kuabudu mizimu huyo ni mkristo feki.


Aidha, padre huyo alisema kuna wengine wanatumia nguvu za tambiko katika miti na milima ili kumaliza matatizo yao na kumsahau Mungu aliyewaumba. Kihiyo alisema kipindi hiki cha Sikukuu ya Krismasi wakristo wanatakiwa kutambua kuwa Yesu Kristo yupo atawasaidia badala ya kuabudu mizimu.

Alisema kuwa kwa kutumia ibada hiyo anawaombea kwa Mungu waumini wanaojihusisha na uganga wa kienyeji na mila za kuabudu mizimu waache mara moja na kumrudia mwokozi wa kweli.

Aliwataka wakristo kuwa na upendo, umoja na mshikamano na majirani ili kumpendeza Mungu katika maisha yao.

Katika hatua nyingine Mchungaji Kiongozi wa kanisa la KKKT Usharika wa Muheza mjini, John Ndimbo, amesema waumini wote wa kanisa hilo wanatakiwa kutubu dhambi zao kipindi hiki cha kuzaliwa Yesu Kristo.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana mtaa wa Madaba wilayani Muheza, Paul Luhinga, aliwataka waumini kuwa watulivu hata kama wanashida na sio kulalamika kila mahali.



Mbunge wa Musoma Vijijini Mkoani Mara, Profesa Sospeter Muhongo, akichangia hoja juzi, katika kikao cha kujadili mikakati ya kuleta maendeleo, kilichoshirikisha wadau mbalimbali wakiwamo wabunge wa mkoa huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge akerwa mchango wake kutotambuliwa

**Na Sabato Kasika**

MBUNGE wa Musoma Vijijini mkoani Mara, Profesa Sospeter Muhongo, ameomba mchango wake na wananchi katika miradi mbalimbali ya maendeleo jimboni mwake utambuliwe.

Prof. Muhingo aliyasema hayo, katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa mjini Musoma juzi na kufafanua kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma imekuwa haitambui anachofanya katika miradi ya maendeleo.

"Nimekaa kimya kwa muda mrefu, lakini sasa inabidi niseme, kwani mimi na wananchi wa Musoma Vijijini tumekuwa tukichangia miradi ya maendeleo, lakini michango yetu haitambuliki," Prof. Muhongo alisema.

Alifafanua kuwa, kwa upande wa elimu, amekuwa akiendesha harambee ya kuchangia fedha na vitu kwa kushirikiana na wananchi lakini halmashauri haichangii na haitambui michango inayotolewa.

"Pamoja na kikwazo hicho, sijakatishwa tamaa, ninaendelea kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo kwa kushirikiana na wananchi katika jimbo letu la Musoma Vijijini," alisema.

Alifafanua kuwa amefanya harambee nyingi kwa kushirikiana na wananchi, huku halmashauri ikishindwa hata kutoa cheti cha shukrani kwa mchango wake wa maendeleo.

"Mimi na wananchi tumekuwa tukichangia miradi ya maendeleo ikiwamo ya elimu, maji na afya, lakini michango yote haitambuliwi. mambo kama haya yanakatisha tamaa," alisema.

Mbunge wa Butiama ambaye pia ni Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Jumanne Sagini alisema kutokutambua mchango wa Profesa Muhongo ni sawa na kutomtendea haki.

"Binafsi Halmashauri ya Butiama imekuwa ikitambua mchango ninaotoa kwa kushirikiana na wananchi na inaendelea kututia moyo kwa kazi nzuri tunayofanya jimboni," alisema Sagini.

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda alisema, Prof. Muhongo amekuwa akifanya jitihada mbalimbali za kuchangia shughuli za maendeleo, na kwamba ni muhimu mchango wake utambulike.

"Taarifa za mbunge huyu nimekuwa nikiziona kila anapozituma zikiwamo za harambee mbalimbali, hivyo kutotambua mchango wake si jambo jema," alisema Mtanda.

# 'Wakumbukeni wenye uhitaji nao wafurahie sikukuu'

**Na Jumbe Ismailly,** IKUNGI

KATIKA kuadhimisha Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, jamii imeshauriwa kuwakumbuka watu wenye mahitaji maalumu kwa kuwasaidia misaada mbali mbali ili nao waweze kusherehekea sikukuu kama watu wengine.

Ushauri huo umetolewa na Mwenyekiti wa Umoja wa wananchi wa Wilaya ya Ikungi wanaoishi nje ya Mkoa wa Singida (IDEA), Hamisi Mpinda, walipokuwa wakikabidhi misaada ya vitu mbali mbali kwa wanafunzi wenye mahitaji muhimu Shule ya Msingi Ikungi Mchanganyiko.

Alivitaja baadhi ya vifaa walivyokabidhi katika shule hiyo ni sabuni za unga, madaftari, sabuni za maji na fimbo za watu wenye uoni hafifu.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya ya Ikungi, Dk. Anthony Mwangolombe akinukuu maandiko mtakatifu alisema dini iliyo safi ni ile ya kuwaona na kuwahudumia wahitaji.

"Wahitaji katika shule ya msingi mchanganyiko Ikungi na wengine wote mnachokifanya ni ibada moja kubwa sana mbele ya Mwenyezi Mungu na ukitoa sadaka hatawapungukia katika mahitaji yenu," alisisitiza.

Awali akitoa taarifa ya Umoja huo, Katibu wa IDEA Wilaya ya Ikungi, Getruda Zakaria aliyataja baadhi ya malengo ya umoja huo kuwa ni kushiriki katika harakati za kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama vile elimu,afya,maji na kuanzisha miradi mbali mbali ili kutumisha na au kuinua uwezo wa kiuchumi wa IDEA.

alizitaja baadhi ya changamoto walizonazo kuwa ni kukosa fursa ya kushiriki kikamilifu na taasisi zilizopo wilayani hapo na ofisa ya halmashauri ya wilaya hiyo kutokana na idadi kubwa ya wanachama kuishi nje ya wilaya na mkoa huo.

Akikabidhi misaada hiyo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Katibu Tawala, Rashidi Mohamedi Rashidi aliushauri umoja huo kuangalia uwezekano wa kutanua wigo wa taasisi hiyo hadi iweze kufika katika wilaya zote za Mkoa wa Singida.

Shule ya Msingi Ikungi Mchanganyiko ina jumla ya wanafunzi 833 ambao kati yao wenye mahitaji muhimu, wakiwamo wenye ualbino, wenye ulemavu wa viungo, wasioona pamoja na wenye uoni hafifu wapatao 86.

# Tshisekedi aendelea kuongoza matokeo ya awali

**KINSHASA,** DRC

TUME ya Uchaguzi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, (CENI), imeendelea kutoa matokeo ya awali ya uchaguzi wa rais, yakionesha Rais Felix Tshisekedi anaongoza, akifuatiwa na mfanyabiashara Moise Katumbi.

Matokeo yaliyotangazwa na CENI kufikia jana mchana yanatokana na takriban kura milioni 1.9, kati ya jumla ya wapiga kura milioni 44 waliojiandikisha katika nchi hiyo yenye wakazi zaidi ya milioni 100.

CENI ilisema Tshisekedi mwenye umri wa miaka 60, aliye madarakani tangu 2019 na anayewania muhula wa pili wa miaka mitano, alikuwa anaongoza kwa zaidi ya asilimia 81 ya kura.

Anaelezwa kuwa anafuatiwa kwa mbali na mfanyabiashara tajiri na gavana wa zamani wa jimbo la Katanga Moise Katumbi, 58, akiwa na zaidi ya asilimia 15 ya kura na mtendaji mkuu wa zamani wa mafuta, Martin Fayulu, 67, kwa zaidi ya asilimia moja.

Aidha, inaelezwa kuwa wapinzani wengine karibu 20, akiwemo Denis Mukwege, mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel mwenye umri wa miaka 68, walishindwa kupata asilimia moja.

Hata hivyo, tume hiyo haijatangaza idadi ya watu waliojitokeza kupiga kura katika uchaguzi wa Desemba 20 na 21 mwaka huu, lakini bado imekuwa ikitoa matokeo hatua kwa hatua tangu Ijumaa, ambayo ni pamoja na uchaguzi wa wabunge, mikoa na mitaa.

Vile vile kumetolewa miito ya utulivu na kujiepusha na vurugu, kutokana na malalamiko ya baadhi ya wapinzani waliotishia kuandamana kwa madai ya kukiukwa kwa taratibu za uchaguzi.

Inaelezwa kuwa uchaguzi huo ulipaswa kufanyika siku ya Jumatano pekee lakini uliongezewa siku kwa sababu ya changamoto kadhaa za usambazaji wa vifaa vya kupigia kura. Huku wagombea wa upinzani wakilaani makosa ambayo walidai yaliharibu kura. **DW**

# Kanisa Katoliki DRC lakataa ndoa jinsia moja

**KINSHASA,** DRC

BARAZA Kuu la Maaskofu wa Kanisa Katoliki nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (CENCO), limesema limeamua kwamba halitabariki ndoa ya wapenzi wa jinsia moja.

Maaskofu wa Kanisa Katoliki nchini DRC walieleza msimamo wao jana, kufuatia barua ya Papa Francis iliyowaidhinisha makasisi kutekeleza baraka ya kubariki ndoa ya wapenzi wa jinsia moja.

Katika mahojiano na Radio Okapi, Katibu Mkuu wa CENCO, Askofu Donatien Nshole alifafanua kuwa msimamo wa baraza hilo hauna maana ya kwamba unampinga Papa Francis.

"Hakika, barua kutoka kwa Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani inatoa uhuru kwa maaskofu kutathmini, kwa kuzingatia hali halisi ya kijamii na kitamaduni ya makanisa ya ndani, kama baraka hii rahisi inaweza kufanywa au la ndani ya jumuiya zao za kikanisa," alisema Askofu Nshole.

Aliongeza kuwa kwa CENCO, katika muktadha wa Congo, kubariki ndoa ya wapenzi wa jinsia moja kuna hatari ya kudhoofisha imani ya baadhi ya Wakristo. Na kwamba kwa upande wao ndoa ipo kati ya mwanamume na mwanamke pekee na kwa kawaida iko wazi kwa uzazi.

Kwa mujibu wa CENCO kesi za ndoa za watu wa jinsia moja ni miungano yenye kupotoka ambayo haiingii katika mpangilio wa uumbaji.

Aidha, CENCO inawahimiza waumini wa Kanisa Katoliki nchini DRC kubaki imara katika kushikamana kwao na Kristo kwa kuthibitisha mara nyingine tena maadili ya Kikristo na ya Kiafrika.

"Kanisa bado liko wazi kupokea kila mtu, hata wavuvi," alisema Askofu Nshole

Hata hivyo Jumuiya ya Wapenzi wa Jinsi Moja (LGBT) haijazungumzia chochote kuhusiana na msimamo wa Kanisa Katoliki nchini DRC.

**RFI**



Wajumbe wa Baraza Kuu la Maaskofu wa Kanisa Katoliki DRC. **PICHA: REUTERS**

# Hamas yakataa kusalimu amri Israel yasema vita vitaendelea

**GAZA,** PALESTINA

HAMAS na kundi la Islamic Jihad wamekataa pendekezo la Misri la kuachia madaraka huko Ukanda wa Gaza ili kupatikana kwa sitisho la kudumu la mapigano, huku Israel ikiahidi kwamba vita vitaendelea.

Hayo yalibainishwa jana na vyanzo viwili vya usalama vya Misri kwa Shirika la Habari la Reuters.

Ilielezwa kuwa makundi yote mawili ambayo yamekuwa yakifanya mazungumzo tofauti na wapatanishi wa Misri huko Cairo, wamekataa kuridhia makubaliano yoyote mbali na uwezekano wa kuwaachia mateka zaidi waliotekwa Oktoba 7 wakati vita vilipozuka huko Kusini mwa Israel.

Misri ilitoa mwelekeo unaoungwa mkono na wapatanishi wa Qatar, ambao unahusisha sitisho la vita kwa mabadilishano ya kuachiliwa kwa mateka zaidi, na kupanua makubaliano yatakayohusisha sitisho la kudumu pamoja na kuuondoa utawala huko Gaza ambao kwa sasa inaongozwa na Hamas.

Misri ilitoa pendekezo la uchaguzi wakati ikiihakikishia Hamas kuwa wajumbe wake hawatafukuzwa au kushitakiwa, lakini kundi hilo la Kiislamu limekataa makubaliano ya aina yoyote mbali na kuachiliwa kwa mateka, huku vyanzo vikisema zaidi ya mateka 100 wanaaminika bado wanashikiliwa huko Gaza.

Ilibainishwa kuwa ofisa wa Hamas ambaye aliitembelea Cairo hivi karibuni amekataa kutoa tamko la moja kwa moja kuhusiana na mapendekezo yaliyolenga makubaliano ya muda ya kibinadamu na kuonyesha kuwa kundi hilo limekataa kwa kurudia msimamo wake rasmi.

"Hamas inataka kumaliza uchokozi wa Israel dhidi ya watu wetu, mauaji na mauaji ya kimbari, na tumejadili na ndugu zetu wa Misri jinsi ya kufanya," alisema ofisa huyo ambaye jina lake halikubainishwa.

**ISRAEL VITA VITAENDELEA**

Wakati huo huo, Waziri Mkuu wa Israel Benjamin Netanyahu, aliapa kupanua vita vya nchi yake dhidi ya Hamas huko Gaza, wakati maofisa wa afya katika eneo hilo wakiripoti dazeni ya waathirika katika shambulizi la Israel kwenye kambi ya wakimbizi.

"Tunaongeza mapambano katika siku zijazo, na hivi vitakuwa vita virefu na havijakaribia kumalizika," alisema Netanyahu.

Hata hivyo, maofisa wa afya katika eneo linalodhibitiwa na Hamas walisema watu wasiopungua 70 wameuawa katika shambulio la anga la Israel ambalo lilishambulia kambi ya wakimbizi ya Maghazi.

Jeshi la Israel lilisema linapitia upya mashambulizi yaliyoripotiwa huko Maghazi, huku likirudia ahadi yake ya kupunguza madhara kwa raia katika vita vyake ili kuliangamiza kundi la wanamgambo wa Hamas.

Ripoti zinasema Misri inapendekeza mpango wa kumaliza mzozo wa sasa kwa kusitisha mapigano, kuachiliwa kwa mateka kwa awamu, na kuundwa kwa serikali ya Palestina ya wataalamu wa kusimamia Ukanda wa Gaza na Ukingo wa Magharibi. Pendekezo ambalo halijatolewa jibu rasmi kutoka kwa Israel wala Hamas.

**VOA**

# MLANDEGE KUTUMIA WAPYA MAPINDUZI, YAIHOFIA AZAM

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Mlandege FC wamesema wanatarajia kutumia wachezaji wapya ambao wamepanga kuwasajili katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili lakini wamedhamiria kulibakisha taji hilo visiwani hapa.

**Mlandege FC itaanza kampeni za kutetea taji hilo kesho kwa kuwakaribisha Azam FC kuanzia saa 10:15 jioni kwenye Uwanja wa Amaan.**

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Msaidizi wa Mlandege, Jaala Abdallah, alisema malengo yake ni kufanya vizuri katika michuano hiyo na kuendelea kuipa heshima Zanzibar.

Kocha huyo alisema mapendekezo ya kusajili wachezaji sita ambao atawatumia katika michuano hii ni kukiongezea nguvu kikosi chake ili kibakishe kikombe hicho nyumbani lakini pia kufanya vyema kwenye Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Aliongeza anafahamu michuano ya Kombe la Mapinduzi mwaka huu itakuwa migumu na wao kama mabingwa watetezi lazima wawe na kikosi kipana kitakachosaidia kupambana kusaka matokeo chanya.

"Ninahitaji kuongeza nguvu katika kikosi changu na nafasi ambazo nimezipa kipaumbele katika usajili huu ni kusajili washambuliaji wawili, mabeki wawili, mlinzi mmoja na golikipa mmoja," alisema kocha huyo.

Alisema kwa sasa klabu hiyo iko katika mazungumzo na baadhi ya wachezaji ambao inawahitaji na taratibu za usajili zitakapokamilika, nyota hao watatangazwa.

"Lazima tuchague wachezaji wazuri watakaofanikisha malengo yetu ya kutetea ubingwa wa Kombe la Mapinduzi, lakini watakaohakikisha tunafanya vizuri pia katika Ligi Kuu Zanzibar inayoingia mzunguko huu wa lala salama," alisema kocha huyo.

Kuhusu mechi dhidi ya Azam, kocha huyo alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu anakutana na timu bora yenye wachezaji wazoefu na mashindano ya ndani na nje ya nchi.

"Kama mwalimu lazima kwanza niwajenge wachezaji wangu kisaikolojia ili kutowaondoa mchezoni. Mchezo wetu huu wa kwanza utakuwa mgumu mno, tunakutana na timu ambayo inawachezaji wazuri na wenyeji uzoefu wa mashindano haya yanayoshirikisha timu kutoka ligi tofauti, hivyo lazima tuwe makini ili kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," Abdallah alisema.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Asha Djaffar (katikati), akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Ceasiaa Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam hivi karibuni. Simba Queens ilishinda mabao 5-0. **PICHA: SIMBA SC**

# *Serikali yatakiwa 'kuibeba' riadha*

**Na Jumbe Ismailly,**
IKUNGI

SERIKALI kupitia Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imetakiwa kutoegemea katika mchezo wa soka peke yake na kusahau michezo mingine katika kuweka fursa sawa kwa wanamichezo wote.

Akizungumza katika Tamasha la Kinyaturu la Ikungi, mmoja wa washiriki wa mbio za kilomita 20, Tunu Andrea, alisema huku lengo la tamasha hilo ni kukumbuka na kuthamini walikotoka, lakini anaikumbusha serikali kutoweka nguvu katika mchezo mmoja wakati michezo mingine pia inaweza kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali.

Andrea ambaye ni mwanariadha wa kimataifa alisema katika karne ya sasa michezo yote ni fursa na hivyo serikali haina budi kuithamini na kuipa kipaumbele.

"Kikubwa kinachotakiwa kutekelezwa na serikali kupitia wizara yenye dhamana ya michezo ni kuhakikisha wachezaji wanawekwa kambini na kupewa mahitaji muhimu vikiwamo vifaa ili kujiandaa vyema," alisema mwanariadha huyo.

Naye Mwenyekiti wa IDEA, Wilaya ya Ikungi, Hamisi Mpinda, alisema tamasha hilo litasaidia kuwahamasisha vijana kujifunza na kufahamu mila, desturi na lengo lake ni kupambana na mmomonyoko wa maadili pamoja na kuimarisha afya na kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

Mpinda pia alikabidhi zawadi kwa washindi wa mashindano hayo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Rashidi Rashidi, na kusisitiza michezo inajenga afya hivyo ni lazima utaratibu bora uandaliwe ili wananchi kujilinda afya zao na kujikinga na magonjwa yasiyoambukiza.

## Mtibwa kufumuliwa, nyota wapya kutua

**Na Adam Fungamwango**

ILI KUINUSURU na janga la kushuka daraja, Mtibwa Sugar imesema itasajili wachezaji wenye uzoefu katika dirisha dogo la usajili lililofunguliwa baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Zuberi Katwila, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, alisema licha ya dirisha dogo la usajili kutotakiwa kusajili idadi kubwa ya wachezaji, timu yao italazimika kufanya hivyo ili kujiweka katika nafasi salama.

"Tumepokea ripoti ya mwalimu wetu, ameweka wazi maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi, ametaka eneo la golikipa asajiliwe mwingine, maboresho mengine ni eneo la mlinzi, viungo na washambuliaji, ripoti imesema wanaotakiwa kusajiliwa ni wachezaji bora, wenye uwezo na wazoefu wa ligi, utaona hapo ni usajili mkubwa unatakiwa kufanyika, viongozi wamepokea na watalifanyia kazi, lengo ni kuhakikisha timu haishuki daraja, Mtibwa Sugar ni timu kubwa yenye heshima nchini, ukiondoa Simba na Yanga," alisema Kifaru.

Mtibwa Sugar inaburuza mkia katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imesalia raundi moja tu kumaliza mzunguko wa kwanza, ligi hiyo imesimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi na fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON).

## Chipukizi FC yaliota Kombe la Mapinduzi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAKATI kikosi cha Chipukizi FC kutoka Pemba kinawasili leo Unguja, uongozi wa timu hiyo umesema umejipanga kuonyesha soka la ushindani na kutwaa ubingwa wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayotarajiwa kuanza kesho.

Chipukizi itaanza kampeni ya kuwania ubingwa wa michuano hiyo kesho kwa kuwaalika Vital'O kutoka Burundi.

Akizungumzia na gazeti hili jana, Meneja wa Chipukizi, Mohammed Abbasi, alisema timu hiyo imejipanga vyema kuhakikisha inaweka historia mpya katika michuano hiyo na kulipeleka Kombe la Mapinduzi Kisiwani Pemba.

Meneja huyo alisema timu yao imesajili wachezaji wazuri na 'wakubwa' ambao anaamini watatoa upinzani wa hali ya juu katika michuano hiyo ambayo inashirikisha timu kutoka ligi tatu tofauti za Afrika Mashabiki.

"Najua michuano hiyo ni migumu na kwa mwaka 2024 itakuwa migumu zaidi kutokana na uwepo wa timu kutoka nje ya Tanzania, lakini kwetu tumejipanga kuonyesha upinzani, tutapambana kuhakikisha sisi Chipukizi tunakuwa mabingwa ili Kombe liende Pemba," aliongeza meneja huyo.

## ZISIKUPITE

**TONEY AKARIBIA ARSENAL**
ARSENAL wamewasiliana na wawakilishi wa Ivan Toney wanapofikiria kutoa ofa thabiti kwa Brentford kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji huyo wa England mwenye umri wa miaka 27.(***Rudy Galetti***)

**MBAPPE: SIONDOKI JANUARI**
MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Kylian Mbappe hataki kuondoka Paris St-Germain katika dirisha la Januari licha ya mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 kumalizika mwishoni mwa msimu. (***L'Equipe***)

**BERALDO KUTUA LIVERPOOL**
KLABU ya PSG imefikia makubaliano ya mdomo ya kumsajili, Lucas Beraldo, anayelengwa na Liverpool, huku mlinzi huyo wa kati wa Brazil mwenye umri wa miaka 20 akitarajiwa kuondoka Sao Paulokwa kwa dau la pauni milioni 17. (***Fabrizio Romano via Goal***)

**BUCHANAN ANUKIA MILAN**
INTER Milan ina matumaini ya kuipiku Manchester City katika vita ya kunasa saini ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Canada, Tajon Buchanan, mwenye umri wa miaka 24. (***Gazzetta dello Sport)***

**BARCO AGOMBEWA ULAYA**
KLABU ya Strasbourg inafikiria kumnunua mlinzi wa kushoto wa Boca Juniors na Argentina mwenye umri wa miaka 19, Valentin Barco, ambaye pia analengwa na Chelsea katika dirisha la Januari. (***Evening Standard)***

**ARSENAL YAMTAKA MAIA**
ARSENAL imemwongeza kiungo wa kati wa Sao Paulo, Pablo Maia, mwenye umri wa miaka 21, kwenye orodha ya wachezaji wanaotarajiwa kusajiliwa katika dirisha dogo la usajili la Januari. (***Football transfers)***

**DRAGUSIN ANUKIA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur inamfuatilia, Radu Dragusin, baada ya kutuma maskauti kumtazama mlinzi huyo wa Romania mwenye umri wa miaka 21, akiichezea Genoa dhidi ya Juventus wiki iliyopita. (***Fabrizio Romano)***

**ILING-JUNIOR AGOMBEWA**
ASTON Villa imeungana na Tottenham Hotspur katika vita ya kumsajili winga wa Juventus, Samuel Iling-Junior, mwenye umri wa miaka 20 kwa dau la takribani pauni milioni 17 huenda likatosha kumnasa mchezaji huyo wa kimataifa wa England. (***Football Insider***)

**FELIX KUBAKIA BARCA**
KLABU ya Barcelona imeonyesha nia ya kumbakisha mshambuliaji wa Atletico Madrid na Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 24. (***Goal)***

**TAH ATAMANI EPL**
KLABU ya West Ham imeingia kwenye kinyang'anyiro cha kumnunua beki wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Jonathan Tah, mwenye umri wa miaka 27, ambaye anapendelea kuhamia Ligi Kuu England kuliko Bayern Munich. (***Bild)***

**SOLANKE ATAKIWA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur imeonyesha nia ya kuhitaji huduma ya mshambuliaji wa Bournemouth, Dominic Solanke, mwenye umri wa miaka 26, ifikapo msimu wa joto. (***Sun***)

**NEWCASTLE, JUVE VITANI**
NEWCASTLE na Juventus zitachuana kuwania saini ya kiungo wa Timu ya Taifa ya England mwenye umri wa miaka 28, Kalvin Phillips, kutoka Manchester City mwezi ujao.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA KUTOMWONGEZA MSHAHARA LEWANDOSKI

**Ni kutokana na ukata lakini pia kiwango cha nyota huyo...**

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA imeripotiwa kutaka kuondoa nyongeza ya mshahara wa Robert Lewandowski ya pauni milioni 5.2 katika mwaka wake wa tatu kwenye klabu hiyo msimu ujao.

**Mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Poland alisajili wa na Barcelona kutoka Bayern Munich msimu wa joto wa 2022 kwa pauni milioni 42, kwa mkataba wa miaka mitatu na chaguo la kuongeza mwaka mmoja.**

Kutokana na matatizo ya kifedha ya klabu hiyo katika miaka ya hivi karibuni, mkataba wake ulitiwa saini kwa njia ambayo ingeongeza mshahara wake mwaka hadi mwaka.

Baada ya kupata pauni milioni 17.3 katika msimu wake wa kwanza, anapokea pauni milioni 22.5 muhula huu, na hiyo inatazamiwa kuongezeka kwa pauni milioni 5.2 katika mwaka wake wa tatu.

Lakini kutokana na kutokuwa katika kiwango bora msimu huu, na masuala ya kifedha ya Barcelona yanayoendelea, jarida la Hispania la Sport limeabdika wanatazamia kusitisha nyongeza ya mishahara yake na kuona kama wanaweza kurekebisha mshahara wake unaotarajiwa msimu ujao.

Hiyo ni baada ya Kocha wa Barcelona, Xavi kuripotiwa kukasirishwa na Lewandowski wakati wa mapumziko katika ushindi wao wa mabao 3-2 dhidi ya Almeria.

Baada ya mchezo huo ambao timu hizo zilitoka sare ya 1-1 hadi mapumziko, Xavi alisema: 'Wakati wa mapumziko nilikuwa na mazungumzo magumu zaidi kama kocha. Je, imefanya kazi? Tayari umeiona.'

Mundo Deportivo iliripoti Xavi hakufurahishwa na tabia ya timu yake na kutokuwa na nguvu katika kipindi cha kwanza.

Ripoti hiyo pia inadai kocha huyo hakuridhishwa na kiwango cha Lewandowski.

Kiwango cha Lewandowski kimetiliwa shaka msimu huu licha ya kufumania nyavu mara tisa katika mechi 21 alizocheza za mashindano yote.

Amefunga mara moja pekee katika mechi zake tano zilizopita za LaLiga na Barcelona tayari wamepitwa pointi saba dhidi ya viongozi Girona.



# AFCON, UNITED ZAMVURUGA ONANA

**LONDON,** England

ANDRE Onana lazima afikirie kazi yake anapoamua kama atakosa sehemu ya msimu wa Ligi Kuu England ili kwenda katika fainali ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) hapo Januari, amesema kiungo wa kati wa zamani wa Manchester United na Cameroon, Eric Djemba-Djemba.

Kipa huyo anaweza kukosa zaidi ya mwezi mmoja wa kampeni za United ikiwa atajiunga na kikosi cha Cameroon kwenye michuano hiyo inayofanyika Ivory Coast kuanzia mapema mwezi ujao.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye alimaliza kustaafu soka ya kimataifa mwezi uliopita, amekuwa akichunguzwa wakati wa mwanzo mbaya wa msimu kwa United ambao umewafanya waondolewe Ulaya na kufanikiwa katika kasi ya ndani.

"Tatizo moja kwake ni hata kama atacheza vyema mwezi ujao, kisha ataondoka kwa mwezi mmoja kwenda AFCON," alisema Djemba-Djemba akiiambia BBC Sport Africa, na kuongeza Onana anaweza kuharibu matarajio yake ya kuwa chaguo la kwanza kwa Cameroon ikiwa atabaki Manchester.

"Anajua akienda, labda atapoteza nafasi yake Manchester United.

"Lazima aamue kilicho bora kwake. Anahitaji tu kufanya kile ambacho ni bora zaidi kwa kazi yake."

AFCON itaanza Januari 13 hadi Februari 11, mwakani na Onana anaweza kukosa hadi mechi nne za Ligi Kuu England ambazo United itacheza kulingana na umbali wa Cameroon kwenye fainali hizo.

# Varane mambo magumu United, kuelekea Saudia

**MANCHESTER,** England

RAPHAEL Varane ameripotiwa kufanya uamuzi juu ya uwezekano wa kuhamia Saudi Arabia baada ya kukosa nafasi katika kikosi cha Manchester United.

Beki huyo ametatizika kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara Old Trafford msimu huu, ameanza mara tano tu kwenye Ligi Kuu England, huku mastaa kama Harry Maguire, Victor Lindelof na Jonny Evans, mara nyingi wakianza mbele ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

Hii imesababisha uvumi anaweza kuondoka katika klabu hiyo, huku ikiripotiwa anatakiwa Saudi Arabia pamoja na klabu yake ya zamani ya Real Madrid, ambapo anaweza kuchukua nafasi ya David Alaba ambaye ni majeruhi.

Kuhamia katika Saudi Pro League kunaweza kumfanya kuungana tena na mchezaji mwenzake wa zamani wa Los Blancos, Karim Benzema.

Gazeti la L'Equipe limeripoti wawakilishi wa Varane wamedai kuhamia Saudi Arabia au Qatar ni'mpango wao'.

Varane aliwahi kutangaza atamaliza soka lake aidha Real Madrid, Manchester United au Lens, ambapo alianza maisha yake ya soka.

Mfaransa huyo ana uhusiano mkubwa na wababe hao wa Hispania, akiweka uhusiano na wachezaji na wasimamizi ambao amefanya nao kazi, na hata kuweka nyumba yake huko.

Hata hivyo, hakujawa na mawasiliano kati ya klabu na mchezaji kuhusu uhamisho wa dirisha lijalo la Januari.

Inadaiwa Varane hapendi kubadili klabu katikati ya msimu, lakini anajua hali yake ya sasa ndani ya Manchester United haiwezi kuongezwa kwa zaidi ya msimu mmoja.

Mail Sport iliripoti wiki iliyopita Mkurugenzi wa Soka wa Manchester United, John Murtough, alisafiri kwa ndege hadi Saudi Arabia ili kujadili uwezekano wa kuondoka kwa Varane, Jadon Sancho, Casemiro, Anthony Martial na wachezaji wengine.

Murtough anafahamika kuondoka Saudi Arabia bila kufikia makubaliano juu ya uhamisho wowote, lakini alianzisha uhusiano mpya muhimu kwa United na mazungumzo zaidi yamepangwa.

Varane alijiunga na United akitokea Real Madrid msimu wa joto wa 2021 na kuunda ushirikiano mzuri na Lisandro Martinez msimu uliopita.

Hata hivyo, huku Martinez akikosa mechi nyingi za sasa kutokana na jeraha, Ten Hag hajabaki na Mfaransa huyo ambaye mara nyingi amekuwa chaguo la nne au la tano katika miezi ya mwanzo ya msimu.

Mkataba wa Varane na timu hiyo ya Old Trafford unamalizika ifikapo mwaka 2025, lakini kuna uwezekano mkubwa kutokana na matatizo ya United msimu huu, na kukosa muda wa kucheza kwa beki huyo klabuni hapo majira ya joto kijacho.





# Gerrard njia panda Al-Ettifaq

**RIYADH,** Saudi Arabia

STEVEN Gerrard yuko hatarini kufukuzwa na mabosi wa Al-Ettifaq ya nchini Saudi Arabia kutokana na matokeo mabaya ya timu hiyo.

Kikosi cha Gerrard Al-Ettifaq kimezidi kupata matokeo mabaya baada ya kucheza mechi nane bila ushindi, jambo ambalo limeifanya timu hiyo kushuka hadi nafasi ya nane kwenye msimamo, licha ya matumizi makubwa ya fedha msimu wa joto.

"Steven Gerrard yuko katika matatizo kidogo pale. Wako katika nafasi ya nane kwenye ligi, pointi 26 nyuma ya vinara, bila ushindi wowote tangu Oktoba," liliandika gazeti la Daily Mail.

"Steven amezungumza katika siku chache zilizopita akiomba fedha zaidi za kusajili wachezaji. Hiyo inaonekana ni jaribio ambalo linaanza kwenda vibaya kwa kocha huyo.

"Na ikiwa hilo litaenda vibaya, kama hawezi kupata anachotaka na hawezi kubadilisha mambo, kama atapoteza kazi hiyo, sijui anaenda wapi katika kazi yake."

"Hufikirii kazi aliyoifanya katika klabu ya Rangers ilikuwa nzuri kama ninavyofikiria. Tumemaliza hilo hapo awali lakini hamjamaliza. Ulifikiri kazi aliyoifanya pale Rangers ilikuwa sawa. Nilidhani ilikuwa bora kidogo kuliko hiyo. Alishindwa pale Villa.

"Taji moja kati ya tisa. Kutoelewa kwako hali ya hewa huko huko Scotland. Unajua, alipata sifa nyingi huko kusini, na alistahili kusifiwa, lakini zingine zilikuwa za juu zaidi.

"Amekwenda Saudia na haionekani kuwa sawa. Je, atapata kazi nyingine katika soka? Ikiwa anataka moja basi ndiyo. Kwa nini? Kwa sababu ana wasifu mkubwa. Lakini atalazimika kufanya kazi bila shaka.

HABARI MICHEZO

# DK. MWINYI MGENI RASMI ZANZIBAR HEROES, KILI STARS

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika mchezo maalumu wa ufunguzi wa Uwanja wa Amaan utakaochezwa leo kati ya wenyeji, Zanzibar Heroes dhidi ya Timu ya Tanzania Bara (Kilimanjaro Stars).

Uwanja wa Amaan unafunguliwa rasmi baada ya kukamilika kwa maboresho mbalimbali yaliyofanyika na kuufanya kuwa wa kisasa.

Mara ya mwisho timu hizo mbili zilikutana mwaka 2020 katika mashindano ya Kombe la Chalenji kwa nchi za Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), yaliyofanyika Uganda ambapo Kilimanjaro Stars ilipata ushindi wa bao 1-0.

Mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani ambao hutokana na historia ya timu hizo kila wanapokutana.

Kocha wa Makipa wa Zanzibar Heroes, Salehe Machupa, alisema mchezo huo utakuwa mzuri na mgumu kwa kila upande kwa sababu wachezaji wanafahamiana kutokana na kukutana mara kwa mara katika mechi za ligi wanazoshiriki.

Machupa alisema Wazanzibari wajiandae kuona soka safi na burudani nzuri ambayo walikuwa wakiisubiri siku nyingi na tena timu hizo zikikutana katika ardhi ya Zanzibar.

Naye nahodha wa Zanzibar Heroes, Feisal Salum 'Fei Toto' alisema timu yao imejiandaa vizuri wanatarajia kufuata maelekezo kutoka kwa makocha wao ili kupata matokeo mazuri.

Fei Toto alisema hawatakubali kufungwa katika ardhi ya nyumbani, hivyo matarajio yake makubwa ni kuona wanapata ushindi utakaowapa furaha na hamasa wenyeji.

"Hatuwezi kukubali kufungwa tena na ndugu zetu, hivyo mchezo wa kesho (leo), lengo letu ni tunawapa raha Wazanzibari, hasa kupata ushindi," Fei Toto alisema.

Bakari Mwamnyeto, nahodha wa Kilimanjaro Stars, alisema anatarajia mchezo huo utakuwa mzuri na wa kiungwana ili kuwapa hamasa Wazanzibari kwa ujumla.

"Mchezo huu ni wahisani sio wa ligi wala mashindano fulani, hivyo tutacheza kwa uungwana mkubwa ili kuwapa burudani Wazanzibari na Watanzania watakaofika uwanjani," alisema beki huyo anayeichezea Yanga.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF), Haji Kibabu, alisema maandalizi ya mchezo huo yamekamilika kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na Shirikisho la mchezo huo la Kimataifa (FIFA).



Kikosi cha KMC FC kilichoanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Simba iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam wiki iliyopita. Mechi hiyo ilimalizika kwa sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

## Simba SC yaahidi furaha..

INATOKA UK 24

duzi alisema kikosi chao kinaingia kambini leo na kitafanya mazoezi kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena kwa ajili ya kujiweka tayari na mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka.

"Kikosi kinatarajia kuondoka Desemba 30 au 31, mwaka huu kuelekea Zanzibar, na tayari kwa mchezo wetu wa kwanza dhidi ya Jamhuri utakaochezwa Januari Mosi, 2024.Tutatumia mashindano hayo kujiweka imara na kocha (Benchikha) atapata muda mzuri wa kufanya mazoezi na kukaa na wachezaji wake kuona uwezo wa mmoja mmoja mbali na wale waliokuwa katika majukumu ya timu za Taifa," alisema meneja huyo.

Aliongeza hakuna mchezaji majeruhi mpya zaidi ya Aubin Kramo ambaye yuko katika hatua ya mwisho ya matibabu yake baada ya kukaa nje kwa muda mrefu.

"Phiri (Moses), ameingia katika siasa ambazo kiungo wetu Clatous Chama aliwahi kuingia katika miaka ya hivi karibuni ya kuhusishwa kutakiwa na klabu moja ya hapa nchini lakini kwa miaka yote anaitumikia Simba. Phiri bado ana mkataba na Simba, hatujapokea barua yoyote kutoka kwa nyota huyo, kama anahitaji kuondoka atalazimika kufuata taratibu," alisema Ahmed.

Aliongeza licha ya Chama kusimamishwa, lakini kiungo huyo anaendelea na programu za mazoezi aliyopewa na benchi la ufundi pamoja na kulipwa stahiki zake ikiwamo mshahara wake.

## *Yanga kumtambulisha Msuva Mapinduzi Cup*

INATOKA UK 24

Gamondi alisema ameshaweka wazi anahitaji kuboresha safu ya ushambuliaji ili kufikia malengo yake katika msimu huu unaoendelea.

"Kuna timu nyingi zinahitaji mshambuliaji, Madrid wanahitaji hata Barcelona wanae Lewandowski (Robert), lakini bado wanahitaji mshambuliaji. Yanga inahitaji hata tukiongeza mmoja itabidi na yeye apewe muda na sio kuingia na kuanza kucheza mechi ya kwanza mnataka afunge mabao matatu.

Hapana kila mchezaji anahitaji muda kuzoea ligi na wakati mwingine tamaduni za nchi alizotoka na Tanzania ni tofauti, kuna muda lugha inakuwa inampa shida wachezaji wengi sana," Gamondi aliongeza.

Wakati huo huo, beki wa kulia wa Yanga, Kouassi Yao, raia wa Ivory Coast anaongoza kwa kutoa pasi za mwisho wa ufungaji, 'assist' kwa upande wa mabeki katika Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, Kouassi, aliyesajiliwa msimu huu akitokea Asec Mimosas ya Ivory Coast ana 'assist' tano mpaka sasa, akifuatiwa na beki wa Azam FC, Lusajo Mwaikenda mwenye 'assist' nne.

Wachezaji Paschal Msindo wa Azam FC, Shomari Kapombe na Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' wote wa Simba wana 'assist' tatu kila mmoja huku mabeki wengine, Cheikh Sidibe (Azam ), David Brayson (JKT Tanzania) na Miraji Abdallah na Coastal Union kila mmoja ana 'assist' mbili.

Kikosi cha Yanga kinatarajia kurejea mazoezini leo baada ya mapumziko ya sikukuu ya Krismasi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

## Metacha, Mshery wanukia Azam FC

**Na Saada Akida**

AZAM FC inatajwa iko katika mazungumzo ya kumsajili golikipa wa Tanzania Prisons, Yona Amosi, kwa ajili ya kuongeza nguvu katika kikosi chao kwenye dirisha dogo la usajili.

Taarifa za ndani zinasema Yona amekuwa akihusishwa na Azam tangu tangu msimu uliopita kwa ajili ya kuchukua nafasi ya makipa waliopo, Abdulai Iddrisu na Ali Ahamada.

Hata hivyo pia Metacha Mnata na Abdultwalib Mshery, wote kutoka Yanga pia wanataja kuwa katika mazungumzo ya kujiunga na klabu hiyo tajiri hapa nchini.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Azam, Thabiti Zakaria (Zaka), alisema wataongeza 'mtu hasa' katika nafasi ya kipa kwa sababu walinda mlango waliopo ni majeruhi na watakaa nje ya uwanja kwa muda mrefu.

Zaka alisema wako makini katika usajili watakaofanya na wanaamini watapata kipa mzuri na bora atakayeenda kusaidia kikosi chao ambaye huenda akatoka ndani au kutoka nje ya nchi.


"Tutaongeza wachezaji, kipaumbele chetu ni kipa kwa sababu tuliokuwa nao ni majeruhi wa muda mrefu, kipa wa kigeni si kipaumbele chetu bali tunahitaji nyanda mzuri kuja kusaidiana na makipa wetu kutoka timu ya vijana.

Kuhusu kipa wa Tabora United, John Noble, ni mkubwa sana na namhusudu sana. Lakini hayuko kwenye mipango yetu, na nyanda tutakaemsajili tutanuniwa na watu," alisema Zaka.

Kuhusu maandalizi kuelekea mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Zaka alisema kikosi chao kitaondoka jijini, Dar es Salaam leo kuelekea Zanzibar tayari kwenda kupambana kuwania taji hilo.

Azam watashuka dimbani kesho kuvaana na mabingwa watetezi, Mlandege mechi itakayochezwa kuanzia saa 10:15 jioni kwenye Uwanja wa Amaan.

Michezo
Jumatano Desemba 27, 2023
Nipashe



UK. 21

Barca kutomwongeza mshahara Lewandoski

# Yanga kumtambulisha Msuva Mapinduzi Cup

## ●●● Winga huyo afunguka lolote linaweza kutokea, lakini bado...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

HATIMA ya winga wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Simon Msuva, kurejea katika klabu yake ya zamani ya Yanga huenda ikajulikana kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayotarajiwa kuanza kesho Visiwani Zanzibar, huku nyota huyo akisema lolote linaweza kutokea.

Taarifa zilizopatikana jijini, Dar es Salaam zinasema Msuva ameshaachana na JS Kablie ya Algeria, na sasa yuko huru kujiunga na klabu nyingine.

Uamuzi wa kutangaza usajili wa nyota huyo huko Zanzibar ulitolewa na Rais wa Yanga, Injinia Hersi Said, ambaye pia alikariri klabu yake itamtambulisha mchezaji ambaye si mgeni hapa nchini katika mechi yao ya kwanza ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema tayari wameshakamilisha mazungumzo na nyota huyo ambaye yuko nchini akifanya mazoezi na kikosi cha Taifa Stars na kinachosubiriwa ni wakati huo sahihi waliopanga.

"Tulitaka kutangaza mchezaji mpya, lakini tumeahirisha, Rais wa klabu akashauri kuwa ni bora tukamtangaze kwenye Kombe la Mapinduzi, mchezo wetu wa kwanza tutamtambulisha mchezaji ambaye tumemwongeza dirisha dogo.

Wasifu wa mchezaji huyo si mgeni sana masikioni mwa watu, hata tukimtangaza kila mmoja atakuwa anamfahamu, ni zawadi kwa Wazanzibar watambue kuna 'chuma' tunakwenda kukishusha, mchezaji bora wa viwango vya juu," alisema Kamwe.

Alisema winga huyo ambaye aliwahi kuichezea pia Wydad Casablanca ya Morocco na Al-Qadsiah FC ya Saudi Arabia anakuja kuchukua nafasi ya Hafiz Konkoni anayetarajiwa kupelekwa katika timu nyingine kwa mkopo au kuvunja mkataba wake.

"Huyo straika anakuja kuchukua nafasi ya Konkoni ambaye kama si kumtoa kwa mkopo basi tutasitisha kabisa mkataba, tuachane naye kwa wema.

Kocha Gamondi (Miguel), ametuambia usajili mkubwa utafanyika dirisha kubwa msimu utakapomalizika," alisema Kamwe.

Msuva alikiri Yanga inafanya mazungumzo naye lakini hakuna muafaka wowote ambao umefikiwa kwa sababu anafahamu Gamondi hana shida na winga na mahitaji yake ni kupata mshambuliaji.

Msuva alisema hata hivyo yeye kazi yake ni kucheza mpira na lolote linaweza kutokea kutokana na uzoefu mkubwa alionao katika kazi yake.

"Yanga ni moja ya timu kubwa, lakini niseme tu nimepokea ofa nyingi, bado ninatamani kuendelea kucheza soka nje ya Tanzania. Hata hivyo lolote linaweza kutokea," alisema Msuva.

Kwa upande wa

INAENDELEA UK 23




# Simba SC yaahidi furaha Zanzibar

**Na Saada Akida**

WAKATI Bodi ya Wakurugenzi ya Simba iliyoko chini ya Mwenyekiti, Salim Abdallah (Try Again) imepokea ripoti rasmi ya mapendekezo ya wachezaji wanaotakiwa kusajiliwa katika kipindi cha dirisha dogo, klabu hiyo imetamba inakwenda kuwapa furaha mashabiki wake katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Ripoti ya benchi la ufundi imeweka wazi inahitaji kusajili wa wachezaji wapya kati ya watano na sita ili kuimarisha kikosi chao kinachowania ubingwa wa Ligi Kuu Bara na kinashiriki hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Nyota wapya wanaotakiwa Simba ni wa nafasi ya kiungo mkabaji, beki wa kati na mshambuliaji.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema tayari Wekundu wa Msimbazi wamemnasa mlinzi wa Mtibwa Sugar, Ladack Chasambi, na kumpa mkataba wa miaka mitatu.

Akizungumza na Nipashe jana,Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema tayari Kocha Mkuu, Abdelhak Benchikha, amekabidhi ripoti yake ambayo imeainisha maeneo anayotaka kuboresha katika kikosi chake.

"Viongozi wamepokea mapendekezo hayo na kuanza kufanyia kazi, ni kweli tunahitaji wachezaji kuimarisha kikosi chetu, tuliokuwa nao si wabaya bali wanahitaji kujituma na kujitoa kitu ambacho tunakikosa katika timu yetu.

Tunatarajia kuongeza mashine ambazo zitakuja kusaidiana na hawa waliopo, kama tutafanikiwa kukamilisha usajili wa nyota wapya mapema wataungana na timu Visiwani Zanzibar katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi," alisema ofisa huyo.

Kuhusu maandalizi ya michuano ya Kombe la Mapin-

INAENDELEA UK 23

9 770856 541002 >